

MSIOGOPE

 Asante Ndugu...?...Asante sana.

² Asanteni, marafiki. Hilo linanifanya tu nijisikie nimekaribishwa maradufu. Hakika ninathamini hilo. Nami, kwa niaba ya Ndugu Borders, na Ndugu Mercier, Ndugu Goad, Billy Paul, mimi mwenyewe, tunataka kusema ya kwamba huu umekuwa ni mkutano mkuu kwetu. Sijafanya mkutano katika sijui ni lini, ambapo Roho Mtakatifu alionekana tu kutoa uhuru kwa karibu chochote, na uhuru mkuu wa kunena, nao wahudumu wanajua hilo linamaanisha nini, ushirikiano mkubwa sana nyuma yenu, mbele yenu.

³ Na ni vibaya sana kwamba hatukuwa na mji mzima huku wapate kuona yale Bwana aliyofanya. Lakini Yeye kamwe... Mimi... Roho Mtakatifu akitoa maono kote jengoni upesi sana, mpaka kusema kweli, ingenibidi kugeuza kichwa changu wakati mwingine, mpaka nipate tu nguvu za kutosha kuendelea mbele kidogo. Imani ye—yenu kuamini, sasa, kamwe msiiache ife.

⁴ Sasa, tunataka kuishukuru hii shule kwa kuturuhusu kutumia ukumbi huu, tunataka kumshukuru mlinzi hapa, mwangalizi, na halmashauri yote ya shule. Na bila shaka tunaomba ya kwamba Mungu atawatoa wanafunzi wengi maarufu kwenye shule hii hapa. Na watu wote walijishirikisha, kwa wadhamini wetu, na wale waliojishirikisha, kwa walei wote kwa kutusaidia kulipia gharama zetu, nafikiri kila kitu kililipiwa. Na hilo tu ndilo linalohitajika, matumizi kulipiwa tu, hilo tu ndilo tunalohitaji, nami mwenyewe, ninapata m—mshahara.

⁵ Ninataka kuwashukuru kwa sadaka ya upendo na sadaka ya umishenari mliyochukua, hiyo huenda moja kwa moja kwenye mfuko huo. Hata sijui, kamwe siangalii pesa zozote mikutanoni, katibu wangu hushughulikia hayo. Zote zinawekwa benki na kuwekwa kando, zikaongezeka mpaka nitakapopata za kutosha kwenda ng'ambo.

⁶ Ndipo ninapoenda ng'ambo, ili kuhakikisha kwamba pesa hizo zinatumika vizuri, ninazichukua mwenyewe. Nami ninahudumu pamoja na huduma ambayo imekuwa mumu humu kwenu nyote, kote ulimwenguni. Na siku moja, huko katika ile Nchi nyingine, ambako kutakuwako, vema, mamilioni watakuwa wakikusanyika kwa sababu ya ushirikiano wenu wa kusaidia kunipeleka mahali pengine, ninatumaini ya kwamba kutakuwako na makumi ya maelfu ya makafiri ambao kamwe wasingemjua Yesu Kristo pasipo ninyi kunisaidia kwenda.

⁷ Sasa, labda wewe, Mungu kamwe hakukuita uende, bali ulitoa sehemu ya riziki yako ili niweze kwenda. Nami ninaenda

kufanya yote niwezayo, na kuwaahidi, kwa neema ya Mungu, kila senti yake itatumiwa kwa uchaji tu iwezavyo kutumika. Hata kutoka kwa zile senti kumi na tatu ambazo maskini mpenzi wangu jana usiku alitupatia, kufikia kiasi kikubwa zaidi cha pesa zitashughulikiwa vizuri, na kutumiwa vizuri sana kadiri tujuavyo.

⁸ Sasa, wadhamini wetu kanisani, mmoja wao ameketi sasa hivi, Bw. Sothmann huko nyuma, na hao wengine ni Wakristo wazuri, kama yeye, nao wanahakikisha hilo, ya kwamba fedha hizi zinatumiwa kwa yale ziliyokusudiwa, zinaenda kwenye misheni za kigeni kusaidia kuujenga Ufalme wa Mungu. Mle ndani, ninapoingia . . .

Unasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa Assemblies.”

Mwingine anasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa Foursquare.”

⁹ Kumbuka, ndugu yangu, dada, pesa hizo huingia moja kwa moja kanisani mwako kule, pia, kwa sababu siwakilishi madhehebu yoyote, wote wanakusanyika kama wafanyavyo hapa. Mnaona? Na—na waongofu wanapokuja, kanisa lolote wanalotaka kuhudhuria, haijalishi kwetu, maadamu tu wao ni wa Injili yote, Wakristo waliozaliwa mara ya pili.

¹⁰ Na kwa hiyo, kwa njia hiyo tu—tunafanya kila tuwezalo kwa uchaji, tukijua ya kwamba itatubidi kujibu kuanzia zawadi iliyo ndogo sana, hadi iliyo kubwa zaidi kwenye Siku ya Hukumu, nami nataka nionekane kuwa wakili mwema wa kazi ya Bwana kwenye Siku hiyo.

¹¹ Na bila shaka tunawashukuru kila mmoja wenu kwa yote mliyofanya, kwa ajili ya imani yenu. Niliona siku hizo usiku . . . Nilianza kuona huko Marekani, na kama sehemu zingine nyingi, watu huinuka, wakati mwingine unaingia mkutanoni, nao hawakubaliani na yale unayosema, watainuka na kutoka, watoke tu makusudi; sijaona jambo hilo katika mkutano huu. Nami nimeijaribu subira yenu ya kuendelea hadi saa nne, na watu wameketi moja kwa moja kanisani, joto, wakijiipepea, wanaketi papo hapo mpaka kwenye maombi ya mwisho, jambo la mwisho linapomalizika mimbarani, huo ni uaminifu. Mungu awabariki ninyi watu.

¹² Sijui, natumaini nitawaona tena, nisipowaona, yale niliyowaambia jana usiku kuhusu Mahali pale, Mungu na ayajibu maombi yangu, na kila mmoja wetu tukutane Huko. Ninawapenda sasa, nanyi mnanipenda, bali hatujui ni kitu gani mpaka tutakapofika Huko, na hiyo ni kweli.

¹³ Ninatumaini ya kwamba kama nikija tena kwamba huduma mpya ninayotaribu kuingiza kwenye mkutano sasa, itakuwa ikifanya kazi kikamilifu kama hizo zingine wakati huo.

¹⁴ Baadhi yao waliniambia huko nje, dakika chache zilizopita, ya kwamba yule mtoto mchanga tuliyemwombea jukwaani

Jumapili alasiri alikuwa hapa. Kama sijakosea, maskini mama huyu hapa mwenye nywele za rangi ya shaba: Je, huyo mtoto mchanga yuko afadhali? Nina furaha sana kwa jambo hilo. Hilo ni zuri. Kasema kilikuwa kinapona sasa, kinakauka, kinakuwa kigaga.

¹⁵ Sasa, hivi hatuna shukrani kwa ajili ya jambo hilo? Madaktari wasingeweza kukifanyia lolote. Laiti mngalijua! Ugonjwa huo huenea usoni kote na kuula tu, mnaona. Lakini sasa ni uponyaji na magamba yanakuja mahali hapo, napo panapona, tunashukuru.

¹⁶ Hili halitawaaibisha. Kulikuwa na...Maskini huyo mama alishangaa ni kwa nini jambo moja lilisemwa jukwaani kuhusu mahali alikotoka. Mnaona, Roho Mtakatifu...Mara baada ya huo mkutano, nilikuwa nikitembea barabarani na ni—nikakutana nao, na kuuliza...Mbona, kasema, “Hakika, hiyo ni kweli, huko ndiko unakotoka, wewe mwenyewe. Lakini ulipoolewa, ulihamia mahali pengine, ama chochote kile kilichokuwa kule.” Ndipo akaliona.

¹⁷ Unaona kile ibilisi anachojaribu kukufanya ufanye? Unaona? Mtoto huyo mchanga asingalikuwa akipata afya kama ungaliendelea kuwazia hilo, unaona. Lakini kama ukiamini, kama tu ni kamilifu vya kutosha kusema mambo kikamilifu, ni...litakuwa kamilifu katika uponyaji, pia.

¹⁸ Aminini tu mambo yote, lolote ambalo Mungu amesema, liamini tu, kwa sababu sio mimi, enyi marafiki. Kumbukeni, kama sitawaona ninyi nyote tena, wengi wenu, mpaka nitakapowaona kwenye ile Hukumu, hayo maono, hiyo Nguzo ya Moto na Nuru ni kweli, mnaona, Hiyo ni kweli.

¹⁹ Sasa, mimi ni mtumishi duni wa Bwana, ninafanya makosa mengi sana hata ninajionea aibu. Siyafanyi makusudi, bali na—nafanya mambo ambayo sipaswi kufanya, kama vile, huenda nikasema, “Njoo, ukamwombea huyu.”

“Vema, naja moja kwa moja hapo na kumwombea huyu.”

“Huyu *hapa* mwingine, huyu *hapa* chini, *hapa* chini.” Ninasahau jambo hilo, simaanishi kufanya hivyo, simaanishi kuwa hivyo.

²⁰ Halafu kuna mara nyingi natamani ningalisimama muda mrefu zaidi mstarini wakati huo upambanuzi unapoendelea, lakini linaniua tu, kamwe siwezi kabisa kufanya hivyo.

²¹ Na nilipoona ono hilo hivi majuzi asubuhi, niliangalia, nikawazia, “Mungu, jalia mtu fulani anishikilie.” Ndipo nikaanza kuwazia, “Naam walifanya hivyo wakati mmoja, nami sikwenda hudumani kwa miezi minane.” Mnaona, nisingeweza kujua wakati mtu yeyote aliponijia, kama ilikuwa ni ono au la. Unaona, hu—huwezi...unaninii tu...kamwe hutaweza

kuwafikia wote, tunajua hilo, lakini tunaweza kufanya kila kitu tuwezacho kufanya kusaidia.

²² Kwa hiyo kutoka hapa tutaenda California hadi Lakespring...Lakeport, Lakeport, California, kwa ajili ya juma lijalo. Juma lijalo tuko hapa juu Yakima, Washington, usiku mmoja huko Tacoma, tunapopitia. Kisha tuingie Summer Shade, Kentucky, na kuendelea mbele, zaidi na zaidi. Na mara niwezapo, nitakuwa nikienda Ujerumani, na Uswisi, Afrika, India, na kushuka kwenda Australia, na Melbourne, Sydney, na New—na New Zealand, kote ulimwenguni. Iweni mkiniombea.

²³ Nawaombeni kibali kimoja zaidi: Mtaniombea wakati nimeondoka? Mnaona, mpaka tutakapokutana, niombeeni. Nami nitakumbuka, wakati changamoto kuu mbele ya watu watakatifu huko India, wale wachawi huko Afrika, ndani kabisa barani ambako, huko Australia na kote, ambapo hao makafiri wapagani, watakuja moja kwa moja na kukupa changamoto, nao watakapotoa changamoto yao, nitakuwa nikikumbuka ya kwamba huko Maporomoko ya Klamath kuna kundi la watu wanaoniombea. Nami ni—nitajua ya kwamba Mungu atayasikia maombi yenu. Nami ninahitaji maombi yenu, watu wanaoomba ndio wanaonishikilia.

²⁴ Nilipokuwa mvulana mdogo, sikuwa na makao, mwajua. Sikusudii kumfedhehi baba na mama yangu, bali mmesoma hadithi ya maisha yangu. Hakuna mtu...Daima niliwapenda watu, nilitaka watu wanipende, wala hakuna mtu angezungumza nami. Ningekuwa nimesimama mtaani kama kijana mwanamume, mtu fulani aje, nami ningekuwa nikizungumza na mtu fulani, kama kulikuwa na mtu mwingine yeyote wangeweza kuzungumza naye, wangeniondokea, kwa sababu ya ule msingi, baba yangu kunywa pombe na kuuza pombe haramu, na kadhalika.

²⁵ Kwa hiyo, na—nachukia kusema hivyo, bali si—si... nitatumaini...Baba yangu alifia mikononi mwangu akimsifu Mungu. Kwa hiyo, na—na—natumaini ya kwamba haionyeshi chochote. Lakini mnaona, ukweli, kama ni jambo baya kwangu, hebu niliseme, kwa vyovyote vile, kwa sababu ni kweli. Mnaona?

²⁶ Ninii tu, hiyo—hiyo ndiyo sababu ninaiamini Biblia. Kwa kuwa, kama sikuisoma ila wakati mmoja, ama kuiangalia, wakati lilipozungumza juu ya Lutu kuishi na binti zake, na kadhalika namna hiyo, haitumii mbinu yoyote, Hiyo inasema kweli. Mnaona? Sasa, wanaposema George Washington hakusema uongo kamwe, hiyo ni historia, sijui hilo, lakini inapofikia jambo *Hili*, inasema kweli, kama ni zuri au baya, inasema vivyo hivyo.

²⁷ Hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa. Kama ni mbaya, siku moja itakuwa kwenye kanopi za anga, kwa vyovyote vile, kwa hiyo afadhali tuungame sasa, na kusema ya kwamba

hivyo ndivyo ilivyokuwa. Mnaona? Kisha uwe mwaminifu. Kamwe hujawahi... Kamwe huwezi kumtumikia Mungu kwa usahihi mpaka uondoe kila kitu kidogo njiani, ambapo unaweza kusimama huru.

²⁸ Ninawezaje kutoka kwenye mlango huo isipokuwa ninaelewa, na nina ufahamu mzuri ya kwamba ninaweza kutokea kwenye mlango huo? Ndipo basi kwa imani, ninatokea mlango huo. Mnaona? Hivyo ndivyo tu uwezavyo. Kama kuna kitu chochote njiani mwako kinachokuzuia, kamwe huwezi kufanya hivyo, kwa sababu kitu hicho kinainuka moja kwa moja mbele zako wakati wote. Unaona?

²⁹ Na kwa hiyo uwe mwaminifu, mkweli, umtumikie Mungu kwa moyo wako wote, “tukiweka kando kila dhambi, ituzingayo kwa urahisi, upate kupiga mbio, kwa subira kwa mashindano yaliyowekwa mbele yako, tukimtaazama Mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu, Bwana Yesu Kristo.” Hiyo... Tazama, Yeye ni Mfano wetu.

³⁰ Sasa, kama nikiweka jiwe la kujikwaa njiani mwako, usiache hilo lizuie wokovu wako na Kristo. Kama mchungaji wako, yeye ni mwanadamu, kama akiweka jiwe la kujikwaa, usiache hilo likuzuie hata kidogo. Jambo unalotaka kufanya ni kuweka imani yako kwa Mungu na kumwagalia Yesu Kristo kama Mfano wako, Yeye ndiye Mfano wako, Yule mkamilifu.

³¹ Sasa, mimi... Kila mmoja wenu, asanteni tena. Na sasa, tuna—tunaweka wakati huu alasiri ya leo... Zaidi sana, tulikuwa na wito wa madhabahuni jana usiku, nami ninatumaini ya kwamba kila mtu wa thamani aliyompokea Bwana Yesu katika mikutano hii utachukua ushirika wako pamoja na baadhi ya makanisa haya, kwa sababu wao—wao wanaamini katika hili, wasingekuwa wakiniweka hapa juu kama hawakuamini katika huduma hii.

³² Sasa, huduma yangu imeshuka kidogo sasa, kwa sababu inabadilika Marekani kutoka moja hadi nyingine. Na kama mmeona jambo hilo, ya kwanza ilikuwa ni ishara ambayo watu waliitazama, ya pili ilikuwa ni ishara ambayo Mungu pekee, Mwenyewe, angeweza kufanya, sasa, kwenye huduma hii ya tatu, inaiweka moja kwa moja mkononi mwa watu tena. Mnaona? Kama watakuja na uaminifu huo, hapana shaka hata kidogo, wamwagalie Roho Mtakatifu, anajiendesha Mwenyewe, ananijia na kuwaambia hasa, anawaponya papo hapo. Mnaona? Lakini hawana budi kuja, si kwa imani ya mhemuko, bali kwa imani thabiti inayoamini kwamba ni kweli. Mnaona? Mungu hulirudisha moja kwa moja mkononi mwa mtu binafsi tena, kwa sababu haina budi kuwa hivyo, maana hakuna nguvu ndani ya mwanadamu kuponya.

³³ Nayo mambo haya ambayo nimewaambia habari zake, wale kuchakulo, kuhusu ku—kuponywa kwa watu hao, na

mambo hayo, Mungu Mbinguni anajua ya kwamba kila neno la hayo ni kweli kadiri nijuavyo kulisema. Hiyo ni kweli. Na kwa hiyo ninajua ya kwamba mbele yangu tu sasa, kuna huduma kuu kuliko niliyo nayo, bali itawachukua watu kidogo tu. Watakapoanza kuiamini, itaanza kufanya kazi. Ninaonaje maono huko nje juu ya kusanyiko kule? Ni vipi? Ni kwa sababu wewe mwenyewe unafanya hivyo. Mimi sifanyi hivyo, ninyi hufanya hivyo.

³⁴ Sasa, nina shaka kama, yeyote wenu amewahi kuona ono halisi, ameniona nikipata ono halisi. Mke wangu angeweza kuwaambia jinsi ilivyo. Wakati mwingine mimi hulala kwa saa kadhaa bila kupumua hata kidogo au, naye daktari anaweza kuchunguza, asione pigo lolote la moyo, ukipiga kiberiti na kukishikilia karibu na pua yangu *hivyo*, hakuna pumzi kwa saa moja au zaidi, lakini hiyo ni katika ono halisi. *Hili* ni kitu kama ono, bali mnalisababisha.

³⁵ Hebu nininii...A—afadhali niliache, tuna wakati mwingi kupita kiasi. Nilikuwa nikitaka kujaribu kuwaelezea vizuri nijuavyo. Ni sawa? Hapa, hakuna mtu anayeweza kulielezea kamwe, kwa sababu halielezeki, lakini hili hapa vizuri nijuavyo mimi. Nitamchukua ndugu yangu mhudumu, aliye hapa jukwaani. Vema. Sote tunaenda kwenye kanivali kubwa, ama, nasema sarakasi. Hivyo ndivyo nilivyo zoea kufanya wakati moja ingekuja mjini ningeninii...ingetubidi kuchungulia kwenye shimo la kifundo mahali fulani, tuiangalie, maana tusingeweza kuingia ndani.

³⁶ Sasa, tutasema ya kwamba—ya kwamba sisi sote tuko kwenye sarakasi hii kuu, nasi hatuwezi kuingia. Basi ikawa kwamba, kwamba Mungu alinifanya mtu mkubwa, mrefu mno, Naye akamfanya ndugu mwingine mtu mfupi, mnene. Sasa, hatuwezi kujizuia jinsi tulivyo. Yesu anasema, “Ni nani akijisumbua aweza kuongeza mkono mmoja kwenye kimo chake?” Huwezi kufanya hivyo. Mungu anakufanya tu kile ulicho.

³⁷ Hapo ndipo ninapotofautiana kidogo na ndugu zetu wa Vuli, ama, ndugu wa Mvua ya Vuli, kwa kujaribu kuwekea watu mikono na kuwafanya manabii, na kadhalika namna hiyo; Mungu huweka Kanisani. Mnaona? Kama mwanadamu akifanya hivyo, ni kama tu kumchagua askofu, ama kuchagua kitu kingine, inafanya kazi kwa nadra, bali Mungu anapomweka, ni kujua Kwake tangu zamani; kwa kujua tangu zamani Yeye alitangulia kuona kila kitu.

³⁸ Nyote mnaamini ya kwamba Mungu hana kikomo? Vema, kama Yeye hana kikomo, Yeye alijua kila kiroboto ambaye angekuwapo duniani, ni mara ngapi angeyapepesa macho yake, na angetoa kiasi gani cha shahamu, kabla ya kuwekwa misingi

ya ulimwengu. Sasa, hilo hata lisingeelezea nusu ya kutokuwa na kikomo, isiyo na kikomo.

³⁹ Yeye ni mkamilifu sana, hata alijua kila kitu ambacho tungepata kufanya. Alijua kila wakati, ni ngapi, ukucha wako ungekuwa na urefu gani, na ni mara ngapi ulipepesa jicho lako, na ni mara ngapi ulisogeza kidole chako, kabla ulimwengu haujaanza, kila mtu binafsi. Hilo halina kikomo. Unaona? *Isiyo na kikomo*, kamwe hakuna, halielezeki, kwa hiyo huwezi kulielezea neno hilo.

⁴⁰ Ni kama tu kwenye—kwenye kamera yako, ama, unapopita umbali fulani, basi u—*unaendelea* tu, ni umilele. Sasa, huyo ni Mungu. Ndipo akajua mambo yote.

⁴¹ Sasa, tutaona Yeye ameweka Kanisani huduma fulani kwa ajili ya nyakati fulani, unaamini hilo. Bila shaka, aliweka.

⁴² Sasa, sote tuko kwenye kanivali, ama, sarakasi, hatuwezi kuingia, hatuna pesa. Sasa, ninamwangalia, tuseme, Ndugu Borders hapa, labda yeye ni mtu mfupi, mnene, ana nguvu vya kutosha, anaweza kuwapelekea tembo maji, labda ajiingize ndani. Vema, nisingeweza kufanya hivyo, maana mimi kwa namna fulani ni mnyonge, bali mimi ni mrefu sana na mwembamba.

⁴³ Basi tunanyemelea karibu na ule uzio mkubwa wa mbao, na—na sote wawili tunasema tungepata shimo la fundo, na liko *huku* juu sana. Vema, Ndugu Borders asingeweza kamwe kulifikia shimo hilo la fundo, lakini ninaweza kama nitaruka. Vema, nitafanya mruko mkubwa mno na kushika juu ya ua kwa vidole vyangu, nitajinyanyua juu, nichungulie kwenye hilo shimo, “Whiu!” Nirudi chini.

Kasema, “Uliona nini?”

“Tembo.”

“Loo, kweli?”

“Uh-huh, naam.”

“Uliona nini tena?”

⁴⁴ Sasa, hayo ndiyo maono mnayoona humu kanisani. Mnaona, nimesimama pale, wewe, mwenyewe unaendesha hilo, unafanya hivyo mwenyewe. Mnapokuwa huko nje kwenye kusanyiko na mnaamini, ninyi wenyewe ndio mnaofanya hivyo.

⁴⁵ Yesu alimwambia yule mwanamke, “Imani yako.” Kwa nini hakuhihi mguso wa hao wengine? Hawakuwa na imani hiyo. Lakini mwanamke huyo mmoja alimgusa, mnaona, “Imani yako imekuokoa.”

⁴⁶ Sasa, muda si muda mwajua wewe. . . Sasa, pale, akisimama jukwaani, huyu hapa mtu, sijawahi kuwaona maishani mwangu. Vema, nifanye nini? Ninaingia katika raha ya nafsi yangu mwenyewe katika karama. Na muda si muda mwajua,

ninamwona huyo mwanamke, ana kansa, “Una kansa.” Loo, jamani, ninaposhuka, kitu kama hicho, kutoka hapa, mnaona, “Whiu! Hilo lilikuwa gumu.”

47 “Naam, nina kansa.” Mnaona? Hilo linapaswa kushtusha kusanyiko hilo lote, lakini halilishtui; hata halimshtui wakati mwingine.

48 “Alibahatisha hilo.” Ninaweza kulihisi papo hapo, mnaona. “Sasa, uliona nini tena?”

Loo, sisi hapa tena, tunaruka juu, ninashikiza vidole vyangu, maana nimepafikia kwa shida tu, ninajinyanyua kwa nguvu.

“Uliona nini tena?”

“Whiu! Twiga.” Mnaona?

“Nina nini tena?”

“Vema, pia una kikohozi cha pumu.”

“Naam, hiyo ni kweli.”

49 Kufikia wakati huo niko karibu kwisha. Mnaona? Sasa, hili hapa limesimama kanisa lote likitaka kujua jambo fulani kuwahusu wenyewe. Mnaona, wanafanya hivyo wenyewe.

50 Sasa, hili hapa lile—lile jitu linakuja, kiongozi wa hiyo sarakasi, “Unafanya nini, mwanangu?”

“Nilikuwa nikiangalia ng’ambo ya ua kupitia kwenye lile shimo la kifundo, nikiwaelezea watu hawa.”

51 Anainama, ananishika mkononi mwake, ananinyanyua hapa juu, anasema, “Unaona *hapa*? Unaona kitu kile *pale*? Hufanyika, kinakuja *huku*. Wavisha Shada la maua wanakuja *hapa*, wanashuka *hapa* chini, nalo linatukia *hapa* chini. Naye mwanamke huyu anarukia *hapa*, anapitia kwenye duara hiyo ya moto. *Huyu* anatoka nje.”

“Loo, hivyo ndivyo ilivyo?”

“Naam.”

“Vema.”

“Hivyo ndivyo ilivyo, mwanangu.”

52 Sasa, huyo ni Mungu akitumia karama Yake; hapa ni wewe ukitumia karama ya Mungu. Hapo kwenye ono halisi ni Mungu akitumia karama Yake, hilo halinisumbui kamwe, halinidhuru hata kidogo, maana nimeketi tu moja kwa moja kwenye kiganja cha mkono Wake, ananionyesha. Hapo ni wakati Mungu anapotaka kutumia karama Yake; na hapo ni wakati unapotumia karama ya Mungu.

53 Siwezi kuitumia, si kwa ajili yangu, ni kwa ajili yenu. Siwezi kujionea chochote. Mnaona? Yote ni kwa ajili yenu. Nina maelfu ya mambo moyoni mwangu alasiri ya leo ninayotamani Yeye anionyeshe, bali Yeye hanionyeshi la kufanya, kunihusu mimi, ni

kwa ajili yenu. Mimi ni mtumishi tu wa umma wa Mungu kwenu. Mnaelewa sasa?

⁵⁴ Sasa, unasema, “Hilo si la Kimaandiko, Ndugu Branham.”

⁵⁵ Naam, ndivyo lilivyo. Sasa ngoja kidogo, Yesu alikuwa akiishi na Martha, na Mariamu, na Lazaro. Mnakumbuka hilo? Ndipo Baba akamwambia Mwanawe, “Nataka kutumia...” Mnaamini Mungu alikuwa ndani ya Kristo? Hakika, alikuwa. Vema. Baba anataka kutumia karama Yake duniani, kwa hiyo anamwambia Yesu, “Wewe ondoka nyumbani, kwa sababu Lazaro atakufa, uwe umeondoka siku nne. Baada ya siku nne, Lazaro atakuwa amekufa, ndipo ugeuke urudi na kumfufua katika wafu.” Hilo kamwe... Kamwe hakusema nguvu yoyote ilimwacha.

⁵⁶ Wakaendelea mbele kwa muda wa siku nne, wakampelekea ujumbe, “Njoo umwombee Lazaro, yuafa.” Akazidi tu kwenda. Wakamtuma mjumbe mwingine, “Njoo umwombee Lazaro, yule umpendaye, yuafa.” Akazidi tu kwenda.

Ndipo baada ya muda, Yeye akasema, “Lazaro amelala.”

“Loo,” wakasema, “kama amelala, anaendelea vizuri.”

⁵⁷ Akasema, “Amekufa. Na kwa ajili yenu, nina furaha sikuwapo.” Kwa sababu wangekuwa wakimjaribu, kumfanya afanye jambo ambalo lilikuwa ni kinyume na mapenzi ya Mungu.

⁵⁸ Basi ndugu, dada, kama sitawaona tena, hayo ni moja ya mapambano makuu sana niliyo nayo. Naangalia moja kwa moja kwenye kusanyiko na kuona mtu fulani ninayejua kwamba hatapona, halafu mtu fulani anajaribu kunifanya nifanye jambo ambalo ni kinyume na mapenzi ya Mungu. Wala siwezi kumwambia mtu huyo, kwa sababu nikimwambia, itawadhuru. Na hivyo ndivyo ilivyo, inakubidi tu kulifungia nafsini mwako na kuliweka, na kuendelea kusonga mbele, ukiomba. Lina—linaua. Halafu basi, muda si muda mwajua, ndipo tutaninii...

⁵⁹ Lazaro, Yeye aliporudi, alienda kwenye kaburi la Lazaro, sikilizeni yale aliyosema, “Baba, ninakushukuru, Wewe tayari umenisikia Mimi.” Mnaona? Mnaona? Tayari alijua jambo hilo. “Lakini ninaomba kwa ajili ya hawa waliosimama hapa.” Ndipo akamwita Lazaro kutoka kaburini.

⁶⁰ Sasa, Yeye kamwe hakusema lolote kuhusu...Huko ni kumfufua mtu baada ya kufa siku nne, na wadudu walikuwa wakiula mwili wake, ndipo mtu huyo akafufuka, akaishi tena, kisha akaenda kula chakula cha jioni pamoja na Yesu. Hiyo ni kweli?

⁶¹ Sasa, huo ulikuwa ni mwujiza mkubwa kuliko maskini mwanamke yule aliyepita na kugusa upindo wa vazi Lake, Akasema, “Nimekuwa dhaifu. Nguvu zimenitoka.” Hiyo ni kweli?

⁶² Mmoja ulikuwa ni Mungu akitumia karama Yake, huo mwingine ulikuwa ni mwanamke huyo akitumia karama ya Mungu, kwa kuwa alisema moyoni mwake, “Yeye ni Mtu mtakatifu, kama nikiweza kugusa vazi Lake, nitakuwa mzima.” Mnakumbuka hilo?

⁶³ Kwa hiyo hilo hapo ono. Sasa inakua zaidi ya hapo sasa, inafikia mahali ambapo watu ambao wameliona wapate kuwa na matumaini na imani, watakuja hapa mbele zangu, nami nitasimama nikizungumza tu nao, na kama watasema tu jambo linalofaa kwa aina ya kweli ya imani, basi upako huo utanijia, na kisha nitawaombea, itatendeka papo hapo. Mnaona? Angalieni tu.

⁶⁴ Basi mkutano huu umekuwa mzuri sana. Kamwe hamjui shuhuda nilizolundika pale kwenye dawati langu, na vitu kama hivyo, ama kwenye, chumbani mwangu, za watu ambao wameandika na kutuma shuhuda za kuponywa, pamoja na watoto wachanga wenye lukemia, na magonjwa ya kila namna, na kadhalika.

⁶⁵ Basi baada ya mimi kuondoka kwa muda mrefu, ninyi wahudumu angalieni makanisani mwenu, mtamwona mwanamke akisema, “Ile shida ya kike niliyokuwa nayo hainisumbui tena, Mchungaji,” ama, “Shida hii ya tumbo niliyokuwa nayo...” “Ugonjwa wangu wa moyo umekwisha kabisa.”

⁶⁶ Nisingeweza kuwaita, nisingeweza kuwaita, ni kote tu kwenye kusanyiko, kila mahali, katika mnyunyizo mmoja tu mkubwa mno. Usingeweza kuwaona wote, usingeweza kuzungumza nao, lakini ni kila mahali tu, wameupata.

⁶⁷ Kama tu nilivyosema juu ya maskini yule msichana mdogo wa Kifini jana usiku. Wewe... Yeye ataligundua baada ya kitambo kidogo, kwa hiyo ni—ni hivyo tu. Na kwa hiyo ninaenda hivyo nikiwa na imani moyoni mwangu, alasiri ya leo, kujua ya kwamba mambo ambayo hatujui chochote kuyahusu sasa, tayari yametimizwa machoni pa Mungu. Kwa hiyo, Mungu awabariki, kwa moyo wangu wote.

Na tuombe dua sasa kwa Mungu.

⁶⁸ Baba yetu wa Mbinguni, baada ya kuwashukuru ndugu na dada zetu kwa ushirikiano wao wote, na wengi wameomba na kufunga, na makanisa yametamani na kujitahidi, na wahudumu wamepitia matatizo makubwa, bali tunakushukuru Wewe, Bwana, ya kwamba katika hayo yote kumekuwa na mambo makuu yaliyotimizwa. Ningejua ya kwamba wahubiri hawatatoka kwenye mkutano huu? Ningejua ya kwamba jambo fulani halijafanywa ambalo litawavuvia watu waliochaguliwa tayari kuhubiri? Tunakushukuru tu kwa hayo yote.

⁶⁹ Wengi wameponywa, utalithibitisha neno la mtumishi Wako, nao ndugu wahudumu na majirani wataona, na kujua ya kwamba maneno yangu ni kweli, ya kwamba ni Maneno Yako ninayosema kwa ajili Yako, kwamba wengi hapa wameponywa wala hawajui bado.

⁷⁰ Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba utatubariki katika kumalizia kwa mkutano huu alasiri ya leo. Mungu, jalia makanisa haya yakue na kufanikiwa katika uamsho mpaka Yesu atakapokuja. Tujalie, Bwana. Yasikie maombi ya watu Wako.

⁷¹ Nasi tunakushukuru kwa ajili ya uchaji na heshima za watu. Na imeandikwa katika Neno Lako, “Kadiri utakavyomtendea aliye mdogo sana,” huyo angekuwa ni mimi, “aliye mdogo sana wa watoto Wangu, umenitendea Mimi.” Na kwa kuwa wameliheshimu Neno ambalo nimehubiri, na ndugu huyu mpendwa akitoa tamshi hilo dakika chache zilizopita katika utangulizi wangu, Mungu, ninaomba ya kwamba utambariki sana, nami ninatambua ya kwamba alinena kwa niaba ya watu, kwa kuwa wote waliitikia kwa shangwe. Nami naomba ya kwamba baraka Zako zilizo na utajiri mkubwa kuliko wote utakuwa juu yao, Bwana. Tujalie.

⁷² Ninaombea huduma zao zote, Bwana, na makanisa yao. Jalia wafanikiwe, na kujenga, na—na kupanuka, na kusanyiko liwe kubwa zaidi, na viti vyote vijae, na madhabahu zijae, na—na uponyaji mkuu wa kimiujiza utafanywa kwa mikono yao. Kwamba umekuwa karibu sana nasi, Bwana, hata inatutia moyo kujua ya kwamba Wewe ungali pamoja nasi.

⁷³ Tunatambua ya kwamba huu ni wakati wa kutikiswa, ambapo Kanisa litafikia uchache, kwa kuwa imeandikwa, “Msiogope, enyi kundi dogo, Baba yenu ameona vema kuwapa Ufalme.” Nasi tunatambua ya kwamba hilo halina budi kufikia mahali hapo, ambapo makapi na ngano hayana budi kutenganishwa. Nasi tunajua ya kwamba huu ni wakati wa kutengana, wakati ulimwengu utaendelea kuwa mbaya zaidi, bali Kanisa litahusika zaidi, na Roho Wako atakuwa mkuu na mwenye nguvu zaidi wakati wote Kanisani, mpaka Kristo na Kanisa watakapoungana pamoja.

⁷⁴ Bwana, tusaide alasiri ya leo kwamba hakutakuwa na mtu mmoja mnyonge miongoni mwetu tutakapoondoka. Sasa ninawakabidhi watu hawa mikononi Mwako, ninajikabidhi mikononi Mwako. Bwana, fanya kazi nasi, tupe kitu cha ziada alasiri ya leo kwenye kumalizia kwa ibada hii ili sote tuweze kukumbuka maadamu tuko hai, pamoja na mkutano uliosalia.

⁷⁵ Tunaomba baraka hii tunapolisoma Neno, litie maji, Bwana. Wewe ulisema, “Neno Langu halitanirudia bure, litatimiza yale liliyokusudiwa.”

⁷⁶ Na wagonjwa wote walio hapa alasiri ya leo, jalia kusiwe na mtu mmoja mnyonge ibada hii itakapokwisha. Mungu na awe

halisi sana kwao, hata weusi wote wa mashaka au ushirikina utaondolewa mioyoni mwao nao watamwona, kikamilifu, Bwana Yesu akitenda kazi miongoni mwa Kanisa Lake. Tujalie, Bwana. Halafu basi, jalia washike imani ya jambo hilo, na watoke hapa pia wanaume na wanawake, wavulana kwa wasichana alasiri ya leo.

⁷⁷ Tunakushukuru kwa ajili ya uponyaji wa maskini mtoto huyu mchanga mpendwa, nami nina furaha sana. Hata hivyo, nilimwambia mke wangu Jumapili iliyopita, “Sina njaa, naomba tusiende kula.” Lakini namtakia heri, alinishawishi mpaka, hatimaye, nikaambatana nao, halafu mtaani, nikakutana na maskini mama huyu. Basi kulikuwa na kitu ambacho Shetani alidhani ya kwamba angeweza kumnyang’anya mtoto huyo wa thamani uponyaji huo, akimfanya mama huyo kutilia shaka kidogo tu pale, kwa sababu kwamba Wewe ulimwambia ya kwamba yeye, mwenyewe, alitoka katika mji fulani, na hivyo ndivyo hasa ulivyomaanisha, ndipo tukisimama kando ya gari, jinsi Roho Wako mkuu alivyorudi tena, na kumfungulia, na kumwambia. Sasa leo hii. . . Ndipo akaamini. Sasa leo hii mtoto wake mchanga anapata afya, tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo, Baba.

⁷⁸ Hao wengine wengi, wote, wengi sana wameponywa, nasi tunakushukuru kwa hilo; watu ambao wameokolewa, tunakushukuru kwa ajili yake. Na jalia kila kitu kiwe kwa heshima na utukufu Wako, kwa kuwa tunayakabidhi yote Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao. Amina.

⁷⁹ Sasa, tutafungua, alasiri ya leo, kwenye Mathayo Mtakatifu kwa ajili ya ujumbe wa kumalizia. Nami na—nawaambia, sina budi kuungama jambo fulani. Mathayo Mtakatifu, mlango wa 14, kifungu cha 27.

⁸⁰ Nami nataka kukiri jambo fulani. Nilifikiri nilikuwa nikihubiri kwa nguvu kidogo. Nami kidogo ninawaogopa wa—wahudumu, mnaona. Mimi ni. . . Wao ni wachungaji, wanapaswa kushuku kidogo, kwa sababu wanalisha kundi la Mungu, na Roho Mtakatifu amewafanya waangalizi. Lakini wakati mimi kwa maskini njia yangu ya polepole, ya kusini. . . Nilikuwa nikifikiri nilikuwa mhubiri muda mrefu uliopita.

⁸¹ Ninakumbuka wakati mimi. . . Baba yangu alikuwa mpanda farasi, naye alikuwa akiwafunza farasi wasiofunzwa, naye alikuwa mpanda farasi hodari. Vema, ninakumbuka wakati ningetoka nje, baada ya kulima mahindi, na kadhalika siku nzima, tungemwingiza ndani maskini huyo farasi wa kulima, Baba angali angekuwa huko nyuma shambani akilima. Tulikuwa na hori la mbao kuukuu la maji. Mnazikumbuka? Gogo lililochimbwa ambapo farasi hunywea, mwajua, kisima cha kale cha chemchemi?

⁸² Nami ningemleta maskini yule farasi mzee kule chini, nintoe hatamu, ndipo tungeninii...Ningechukua tandiko la Baba, mwajua, na kutoka huko nje. Nao maskini ndugu zangu wangeketi karibu na uzio. Nami ningeokota konzi kubwa la magugu miiba, na kuyavuta juu pale, kisha ninakaza mkanda wa tandiko, na kupanda juu yake. Maskini farasi huyo mzee, mzee sana na amechoka sana, mwajua, asingeweza kuiondoa miguu yake ardhini. Angepiga kelele tu, mwajua, ningeitupa kofia hiyo huku na huku, nilifikiri nilikuwa mpanda farasi.

Nikasema, "Jamani! Wananihitaji kwenda magharibi kuwafunzia farasi wao."

⁸³ Nikiwa na umri wa yapata miaka kumi na minane, nilitoka kisiri, nikaenda Arizona, ikawa kwamba nilikuwa huko wakati wa mashindano ya kuendesha farasi. Vema, ninavaa jozi ya surupwenye; sikuzote nilitaka jozi. Za baba zilikuwa zimechakaa, kwa hiyo...Aliumia, kwa hiyo ilimbidi kuacha kupanda farasi. Nami nikawazia ningejinunulia jozi ya surupwenye, ndipo nikatoka na kujivika jozi. Nilikuwa mdogo, hata hivyo, mwajua, na ilikuwa ni mojawapo wa zile za kimagharibi zenye miguu mirefu, na kulikuwa karibu na ngozi ya kutosha sakafuni kutengeneza tandiko. Ilionekana kama mmojawapo maskini majogoo hawa wadogo wenye hayo manyoya, mwajua, imetokeza...Nisingeweza kuvaa vitu hivyo. Kwa hiyo, nilitaka kupeleka pesa za matandiko nyumbani, mwajua, nipande matandiko ya fedha, nanyi mnajua ninachozungumzia. Kwa hiyo nikachukua jozi ya Levi, nikatoka nikaenda kwenye zi—zizi.

⁸⁴ Ndipo wakasema watamleta farasi mtukutu, na kwa hiyo mpanda farasi maarufu atampanda. Nikatulia pale na kuwaangalia maskini hawa makaoboi wote, walioharibika sura, mwajua, walioketi kwenye uzio huu, wakiangalia, nilipanda nikaketi karibu nao. Nikaangalia, niliona ovaroli zao, mwajua, zote za kuteleza na chakavu, yangu, niliwaambia tu ilikuwa ni jozi mpya. Nilikuwa mpanda farasi, kwa vyovyote vile, mwajua, nikawaza, "Nitawaonyesha jinsi ya kuwaendesha farasi hawa huku magharibi. Nitawaelezea jinsi ifanywavyo."

⁸⁵ Nimeketi pale, nikiwaangalia pande zote, mwajua. Ndipo muda si muda mwajua, wakatoka kibandani, jamaa huyu alitoka, juu ya farasi aliyeitwa Homa ya Manjano, chapa kubwa kwenye nyonga yake. Yapata miruko mitatu ama minne na teke au mawili makali sana, ndipo farasi akaenda njia *moja*, mpandaji *nyingine*; pikapu ikamwokota farasi, na gari la kuchukulia wagonjwa likamwokota mpandaji.

⁸⁶ Mtangazaji akapitia hapo, na kusema, "Nitampa mtu yeyote dola mia moja ambaye atampanda kwa sekunde thelathini." Akashuka kupitia pale, naye akasimama mbele yangu, akasema, "Je, wewe ni mpanda farasi?"

Nikasema, “La, bwana.” Hilo liliondolea majivuno *sasa hivi*.

⁸⁷ Nilipokuwa maskini mhubiri wa Kibaptisti, nilikuwa nikibeba Biblia yangu chini ya mkono wangu, mwajua, na kwenda katikati ya mji, ningewaona watu mbalimbali, wangesema, “Halo, Kasisi.” Loo, hilo lilisikika *kubwa*, mwajua. Naam, bwana.

“Wewe ni mhubiri?”

“Loo, naam.”

⁸⁸ Siku moja, kulikuwa na msichana mdogo jina lake Betty Daugherty, mlisoma hadithi hiyo, alieponywa katika huduma yangu. Wa kwanza katika huduma yangu, wakati ilipothibitishwa kwangu kule; naye baba yake alikuwa mhubiri wa Kipentekoste. Nami nikashuka kwenda mkutanoni. Jamani, loo, jamani! Mtu huyo angehubiri, mpaka, hakuhitaji maikrofoni yoyote, angehubiri mpaka angegeuka bluu usoni, akiyagonganisha magoti yake, na kushuka karibu sakafuni, arudi juu akivuta pumzi yake, ungeweza kumsikia umbali wa majengo matatu au manne angali akihubiri.

Mtu fulani kasema, “Wewe ni mhubiri?”

Nikasema, “La, bwana, sivyoo. La, bwana.”

⁸⁹ Maskini njia zangu za polepole, za kusini kamwe haziwezi kuliwazia upesi hivyo, hivyo tu. Inanibidi kwa namna fulani kuchukua wakati wangu na kupenya huku, na kwa namna fulani kumngojea Roho. Nami ni mwenda pole sana, hivyo tu, hao ndugu wa Kipentekoste wangetimua mbio tu na kuniacha. Kwa hiyo, nami kidogo nachelea kusema kuhusu kuwa mhubiri jukwaani wakati najua hao wako nyuma yangu, mwajua, kwa hiyo kuliendea kwa uangalifu.

⁹⁰ Lakini nilipowasikia wakisema kuhubiri juu ya utakatifu, wanathamini jambo hilo, na baadhi ya hao wahudumu wakinipa mikono, na kusema, “Hilo ni zuri, Ndugu Branham, hilo linatupa ujasiri, na kusonga mbele.”

⁹¹ Loo, niliacha kuhubiri yapata, siku tatu zilizopita usiku na nikaanza tu kushuhudia, kwa sababu nilihofia kwamba nilikuwa, huenda nikaanza kuwa mkali kidogo juu yake, mwajua, kwa hiyo ni—nikaliachilia tu. Lakini mimi, wakati mwingine nitakaporudi, nitaendelea kuhubiri, maana ninawajua ninyi ambao mnachukulia na sasafrasi ya mtindo wa kale. Ni wangapi wanaojua sasafrasi ni nini? Aisee, jamani!

⁹² Ni wangapi waliowahi kulala kwenye mto wa nyasi kavu? Ni wangapi wanaotoka Kentucky? Jamani, hiyo—hiyo kweli. . . Hiyo ni Kentu-. . . Mbona, nilizaliwa kwenye mto wa nyasi kavu. Hiyo ni kweli. Nikalalia foronya ya makapi karibu maisha yangu yote. Hatukuwahi kuwa na taa za umeme, hadi hivi majuzi tu.

⁹³ Nami nakumbuka Baba alikuwa akinyoa, angetoa kichala cha makapi kutoka kwenye mahindi, mwajua, alijitengenezea brashi ya kunyolea. Anaenda kwenye beseni ya Mama, anchukua maskini sabuni ya magadi ambayo yeye . . . tulichemsha vitu vya kale na kutengeneza sabuni ya magadi, na . . . ? . . . juu namna hiyo, anaosha kichwa chake, na kila kitu, sabuni ile ile ya magadi, anachukua maskini brashi hii na kuweka mapovu ya hiyo sabuni usoni mwake na kunyoa. Loo, jamani! Laiti ningaliweza kumwona tena hata hivyo, hakika laiti ningaliweza.

⁹⁴ Lakini mshikilie Kristo, ama, hili: acha Kristo akushikilie. Ni kama tu wakati mmoja . . . Laiti ungemruhusu Yeye akushikilie! Sasa, sisi si Kanisa kubwa, hiyo ni kweli, bali ninaamini Mungu anatushikilia.

⁹⁵ Msichana wangu mdogo, Rebekah *pale*, mimi husimulia hadithi ndogo juu yake na Sarah siku moja. Wote—wote wawili ni wasichana wadogo wa Baba, mwajua. Na kwa hiyo, mimi hucheleva huko nje, mwajua, nami ni—ninawapenda watoto wangu, nami nisingeingia mpaka labda majuma kadhaa. Basi ninamkumbuka Rebekah wakati mimi . . .

⁹⁶ Kuzaliwa kwake kulikuwa kumbukumbu ya huduma yangu. Nilimwomba Bwana kama angeniruhusu nikae nyumbani mpaka huyo mtoto azaliwe. Ndipo wakati mimi . . . akazaliwa, nami nikaenda safarini, kisha nikarudi, naye akaanza kunifahamu. Akiisha kuwa na umri wa yapata miezi sita, ama kitu kama hicho, nilifanya mikutano ya St. Louis, na michache ya Arkansas, nikashuka huko chini kusini, na nilipoondoka wakati huo, sikurudi kwa karibu mwaka mzima. Nilipokuja katika siku moja yenye baridi . . . Nasi tulikuwa na vyumba viwili vidogo tulivyokuwa tukiishi, na tulikuwa tumechomeka mfarishi mlagoni na kuusukuma ndani, hali ya hewa ilikuwa karibu sufuri.

⁹⁷ Basi kumfanya huyo mtoto mchanga asinisahau, mama alikuwa ameweka picha yangu *pale*, naye angemwambia Rebekah, naye angesema, “Baba, Baba.”

⁹⁸ Lakini niliporudi, nilikuwa nimepoteza yapata ratili ishirini na tano, karibu nywele zangu zote zilikuwa zimekwisha, nami nikasema, “Jambo, Mpenzi,” aliogopa, akalia, aliniogopa. Mtoto wangu mwenyewe akiniogopa.

⁹⁹ Naye mama akajaribu kusema, “Baba,” naye angeelekeza kwenye picha, *huyo* alikuwa Baba, si *huyu*, hilo nusura liniue.

¹⁰⁰ Hatimaye, nikashika miguu yake midogo, na kuiwekelea kwenye tumbo langu, nikaketi chini, na kuanza kumpapasa, na kumwambia nilikuwa Baba, nami nilikuwa huko nje nikimtumikia Bwana. Ndipo hatimaye, akalaza maskini kichwa chake kifuani mwangu, akalala hapo kwa muda kidogo, naye angeinuka tena na kuiangalia ile picha, halafu ananiangalia tena. Hatimaye, akaridhika ilikuwa ni mimi, mwajua.

¹⁰¹ Wakati dada yake mdogo alipozaliwa, vema, Becky kidogo ni mrefu, mwembamba, mwenye miguu mirefu... Na kwa hiyo walikuwa wakingojea usiku mmoja nje nyumbani, nami nikaingia kidogo nimechelewa. Kwa hiyo basi niliporudi nyumbani, mbona, walikuwa tayari wameenda kulala.

¹⁰² Ndipo kesho yake asubuhi, nilikuwa mchovu sana na dhaifu, maono mengi, nami ningeninii, ningeshekwa na usingizi, wala nisingeweza kulala, nilikuwa nimechoka sana. Ndipo nilipoamka, nikatoka chumbani, mbona, nikaketi huko nje, muda si muda mwajua, Becky akaamka kwanza. "Vema, kumepambazuka, huenda Baba yupo." Huyu hapa anakuja, hizo pajama zikipepea tu. Ndipo alipokimbia, yeye...

¹⁰³ Huyu hapa Sara anakuja, dada yake mdogo, maskini mtoto mchanga *hivi*, amevaa nguo alizoachiwa na Becky. Nadhani watoto wenu hufanya hivyo, pia. Miguu mirefu mno *hivi*, mwajua, nao hawa hapa akiichapusha hiyo miguu mikubwa wakija, na maskini macho yake, ya hudhurungi.

¹⁰⁴ Lakini Becky akaruka moja kwa moja akatagaa gotini mwangu, namna *hii*, na kunikumbatia *hivi*, na kusema, "Sarah, dada yangu, nataka ujue ya kwamba nilikuwa hapa kwanza," hivyo ndivyo baadhi ya makanisa makubwa ya kimadhehebu yanavyowazia, walikuwa hapa kwanza, "nami ninaye Baba wote," alikuwa amesawazika vizuri, miguu yake ilikuwa sakafuni, alijisawazisha vema kabisa, kasema, "Ninaye Baba wote, wala hakuna kilichosalia kwako."

¹⁰⁵ Maskini mtoto Sarah, alikiinamisha maskini kichwa hicho, hayo macho madogo ya hudhurungi yakaniangalia, yametiwa rangi kwa machozi, akaanza kugeuka. Naye Becky alikuwa akijisogeza karibu nami. Nikamwashiria Sarah *hivi* kwa kidole changu, nikachomoa goti langu lingine, naye huyu hapa akaja, hiyo miguu mikubwa ya pajama ikiruka. Akaruka moja kwa moja, akatagaa pajani mwangu namna *hiyo*, nami nikanyosha tu mkono nikamshika kwa mikono yote miwili na kumkumbatia kwa nguvu sana.

¹⁰⁶ Akalala pale kidogo akiegemea kifuni mwangu, kisha akamwangalia Becky, na kusema, "Rebekah, dada yangu," akasema, "huenda ikawa ni kweli kwamba unaye Baba wote, lakini nataka ujue Baba ana mimi wote."

¹⁰⁷ Jambo ndilo hilo. Huenda tusiwe na theolojia nyingi sana, huenda tusijue mengi sana kuhusu jinsi ya kupasua molekuli, ama sisi hatuna umri mkubwa sana, ila jambo moja, maadamu Kristo ana mimi wote, hilo tu ndilo ninalotaka, mnaona. Huenda nisiwe na Yeye wote, mradi Yeye ana mimi wote, Yeye atanisaidia na kunisawazisha, mpaka nitakuwa mkubwa kidogo, nina hakika.

¹⁰⁸ Sasa, katika Neno la kale lililobarikiwa... Loo, ninalipenda Neno! "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.

Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe,” alisema Yesu. Sasa:

Ndipo *mara Yesu akasema nao, akawaambia, MsioCOPE; Jipeni moyo; ni mimi; msioCOPE.*

¹⁰⁹ Hapana shaka ilikuwa karibu kutua kwa jua, ilikuwa ni siku kuu, yenye joto kiasi, naye yule mvuvi mashuhuri, kama tujuavyo, Simoni, jamaa mkubwa, mnene, mwenye upara, mabega mapana, akiisukuma mashua kutoka ukingoni, na hatimaye akaishika, shetri imesukumwa, akapanda mwenyewe, na kuisukumiza majini, akatembea kwenye viti vilivyosalia, kisha akachukua mahali pake karibu na Andrea, ndugu yake.

¹¹⁰ Watu waliokuwa ufukoni walikuwa wakipunga mikono wakisema kwaheri, “Mungu awe pamoja nanyi hata tutakapokutana tena,” na kupunga mikono, na kushangilia sana kwa sababu ya huo mkutano mkuu siku hiyo. Walipoanza kuchukua makasia yao kwa nia moja, wakivuta pamoja... Hivyo ndivyo mnavyousogeza mtumbwi, ni hapo mnapofanya pigo lile lile pamoja.

¹¹¹ Hivyo ndivyo nimesimama katika pengo na ndugu wa Kipentekoste, wakati kila mmoja wetu angeweza kusimama karibu na makasia yetu na kuvuta pamoja na hao wengine, mtumbwi utasonga moja kwa moja upande wa pili. Jahazi letu dogo litavuka bahari ya uhai, ambapo tunaabiri kwenye njia kuu ya maisha sasa. Na hilo ndilo tunalohitaji ni ushirikiano, uratibu, na kuvuta pamoja kwa uthabiti, bila shaka itasogeza mzigo.

¹¹² Basi walipokuwa wakiendelea na safari, loo, baada ya jua kuwa jekundu tayari, likitua, walifikia umbali ambao wasingeweza kumsikia yule wa mwisho akiwaaga, “Kwaheri.”

¹¹³ Nami ninaamini, ya kwamba hapana shaka ilikuwa ni kijana Yohana, kwa kuwa alikuwa ndiye mdogo kuliko wote miongoni mwao wote, hapana shaka kijana Yohana alizirudisha nyuma zile nywele za matimutimu kutoka machoni mwake, na kusema, “Mnajua, nimekuwa nikiwazia tangu alasiri ya leo. Na, loo, jinsi Biblia ilivyo halisi kwangu sasa! Hivi mlimwona, ndugu, mwonekano huo usoni Mwake wakati alipochukua hizo biskuti, na kuzivunja, na kuwalisha hao elfu tano? Kwangu mimi alionekana kama Yehova, amesimama pale.

¹¹⁴ “Naye akawavunja hao samaki na kuwapa, na ninii Yake... Nikasogea karibu na kuangalia, na kumwona Yeye wakati angemvunja huyo samaki vipande viwili, akawapa, halafu wakati aliporudisha mkono nyuma, kungekuwako na kipande kingine cha samaki aliyepikwa pale, mpaka maelfu ya vipande vya samaki vikatokea kwenye kipande hicho cha samaki, tayari kimepikwa.

¹¹⁵ “Nilimwona wakati alipoivunja biskuti hiyo, akawapa, akanyosha mkono tena, na hiyo biskuti ilikuwa nzima tena,

akaendelea tu kuwapa. Kisha nikamwona akiokota vikapu hivyo vyote vilivyojaa chakula.

¹¹⁶ “Mnajua, ndugu, ninaweza kuwahakikishia,” hapana shaka alisema, “kwamba hatujadanganyika, Mtu huyo ana mawasiliano fulani na Yehova, kwa sababu mama yangu, nilipokuwa mvulana mdogo, alikuwa akinisomea hadithi jinsi Yehova alivyonyesha mvua ya chakula kutoka Mbinguni na kuwalisha watu wetu, watu wetu wa kale, walipovuka jangwa. Kwa muda wa miaka arobaini nyikani, Mungu, Yehova, aliwalisha kutoka Mbinguni, akanyesha mvua ya chakula, kilichopikwa, ardhini, kikiwa na asali juu yake. Sasa, Mtu huyu hufanya mambo kama vile Yehova alivyoyafanya.” Amina. Ninapenda hilo.

¹¹⁷ Akasema, “Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi nizifanyazo.”

Wakasema, “Neno la—la—lako si la kweli, unajishuhudia mwenyewe.”

¹¹⁸ Akasema, “Wawili ni shahidi. Mimi ni Shahidi mmoja, na Baba Yangu aliye pamoja Nami ndiye Shahidi mwingine, Yeye hufanya kazi.” Kwa hiyo Yeye hakuwa peke yake. Baba... Alisema, “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi, bali nikizitenda kazi za Baba Yangu, basi kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini hizo kazi, kwa sababu kazi hizo ndizo Baba Yangu.”

¹¹⁹ Sasa, huenda tukasema jambo lile lile. Kama sisi... Kama hamwezi kutuamini kama watumishi wa Kristo, mwaminini Roho Mtakatifu aliye pamoja nasi, akitenda kazi za Kristo, mwaminini Yeye.

¹²⁰ Sasa, kwa hiyo akasema, “Huyo hapana shaka alikuwa na uhusiano fulani na Yehova, kwa sababu Yehova alifanya mwujiza na kuwalisha watu kwa mkate walipokuwa na njaa, naye Bwana wetu, alasiri ya leo, aliwalisha watu kwa mkate na samaki walipokuwa na njaa; hapana shaka ilikuwa ni kitu fulani, mawasiliano fulani aliyo nayo na Yehova.

¹²¹ “Nami nimeridhika, haidhuru kanisa letu linasema nini, haidhuru Mafarisayo wanasema nini, ama Masadukayo, ama yeyote yule, ninajua ya kwamba hatudanganyiki katika Mtu huyu, kwa sababu Yeye hufanya kazi za Mungu. Kazi zile zile ambazo Mungu alifanya, Yeye huzifanya, pia.”

¹²² Ninaweza kuwasikia ndugu kote kwenye meli wakisema, “Amina, Ndugu Yohana, hiyo ni kweli kabisa.”

¹²³ Sasa, hapana shaka ilikuwa ni Mtume Petro wakati huo ambaye kidogo alikuwa kwenye shetri ya mashua, yule mvuvi, kama tunavyomwita, hapana shaka ilikuwa ni yeye aliyesema, “Vema,” akaachilia kasia lake, ameketi karibu na Andrea, akasema, “vema, nitakwambia kilichonishawishi kabla ya

alasiri ya leo, Yohana. Andrea alienda kumwona kwanza, naye akaja akiniambia kuhusu Nabii wa Galilaya, nami nikasema, ‘Loo, Yohana, usichukuliwe na upuuzi huu mwingi unaoendelea siku hizi.’ Kwa sababu unajua kulikuwa na wapinga Kristo kadhaa walioinuka kabla ya kuja Kwake, ulijua hilo, Biblia ilisema hivyo, ya kwamba waliwaita wengi. “Lakini,” akasema, “kilichonishawishi, ninaweza kukumbuka. . .”

¹²⁴ Ndipo ndugu wote wakaachilia makasia yao, kwa sababu ilikuwa tu ni utulivu ule mdogo kabla giza halijaingia, na ule ukungu kando ya milima, wakati wa kupendeza, ndege wote wakiruka juu, wakienda kwenye viota vyao, Mungu alikuwa amewalisha mchana kutwa, nao walikuwa wakikusanyika kwenye viota kwa ajili ya jioni.

¹²⁵ Loo, nina furaha sana kwamba Mungu atawakusanya watu Wake wakati wa jioni, nanyi je? Hapo ndipo Bibi-arusi atakapoitwa. Mlijua hilo? Wakati wa jioni. Hapo ndipo Rebeka na Isaka walipokutana, ilikuwa ni wakati wa jioni.

¹²⁶ Ndipo ndege walipoanza kukusanyika kuingia, hao ndugu wakaacha kuvuta makasia, na walipoacha, Simoni akasema, “Andrea aliendelea kuniambia, ‘Hima, Simoni. Kwea ukamwone Nabii huyu wa Galilaya, Atakufanya umwamini Mungu.’

¹²⁷ “‘Loo,’ nikamwambia Andrea, ‘Andrea, hapana shaka umeingia wazimu. Hakuna kitu kama nabii katika siku zetu.’

“‘Lakini wapo,’ akasema, ‘wapo. Unapaswa kuja.’

¹²⁸ “Siku moja akanishawishi niende. Kwa hiyo, hatimaye, nikakwea, nami ninakumbuka yale baba yangu aliyoniambia. Sasa, baba yangu alikuwa Mfarisayo mkali, mkali sana katika dini yetu, naye alinifundisha Biblia vizuri. Nami ninaweza kukumbuka lile somo, siku moja, tukiketi kwenye gogo kuukuu, ama upande wa mwisho wa meli baada ya kuvuta siku nzima, naye alikuwa anazeeka na ana mvi, naye akanichukua pajani mwake, nami nilikuwa mvulana tu, ndipo akasema, ‘Simoni, mvulana wangu, baba yako amekulea kumwamini Mungu. Nimejaribu kuishi maisha magumu ya dini yetu, Mfarisayo, nami ninakutaka uje ukamtumikie Mungu na kumwamini. Nimengojea siku zangu zote, Simoni, mwanangu, kumwona Masihi akija, ninajua jinsi atakavyoonekana, ninajua kile atakachokuwa ajapo. Nami naona, siamini nitaweza kumwona Yeye.’”

¹²⁹ Na huenda Simoni alisimama hapa, na kusema, “Ninamwona baba yangu mzee akirudisha nywele nyuma kutoka machoni mwake, kama ndevu zenye mvi na nywele, tulikuwa tumevua samaki pamoja kwenye bahari ya Galilaya hapa maishani mwetu mwote, basi akasema, ‘Simoni, mwanangu, huenda ukaishi upate kumwona Masihi. Naye atakapokuja, atakuwa ni Mtu aliyekataliwa. Loo, hatakuwa na wafuasi wengi wa kmfuata, bali atawaita Wateule wa Mungu.

Atawaita, pia Simoni, nimeomba sana kwamba ningemlea mvulana, angekuwa miongoni mwa Wateule wa Mungu.

¹³⁰ “Sasa, Simoni, Masihi ajapo, ninataka ukumbuke, Yeye atashutumiwa, atadhihakiwa, lakini hii hapa ishara ambayo utajua Yeye ni Masihi: Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii, kwa sababu Musa, yule nabii mkuu tunayemfuata, alisema Bwana, Mungu wetu, atamwinua Nabii mithili yake. Sasa, Yeye atakuwa ni Nabii kama Musa, lakini mkuu zaidi kuliko Musa. Unaona? Atakuwa ni Nabii, Mfalme, Kuhani, Mtoa-Sheria, Yeye atakuwa ni Mungu katika mwili, bali Yeye atafanya ishara ya nabii, na hivyo ndivyo utakavyojua ya kwamba Yeye Ndiye wa kweli. Unaona?”

¹³¹ Kisha akasema, “Basi nilipoenda mbele za huyu Yesu wa Nazareti, basi niliwazia, ‘Nitaenda nione ni mwongo fulani. Siamini yale Andrea anayoniambia, ninaamini ameshikwa tu na mhemko fulani.’ Lakini nilipotoka kwenye meli yangu, aliniambia Yeye alikuwa huko juu ufukoni, nami nikapanda juu na kuketi kwenye gogo, nikangojea kumsikia huyu Mgalilaya akinena.

¹³² “Basi alipokuwa akizungumza, aligeuka na kuniangalia. Basi aliponiangalia, nilijua alikuwa tofauti na watu wengine.” Acha tu akuangalie wakati mmoja. “Nilijua kulikuwa na *jambo fulani* kumhusu. Nilipomsikia akinena, Yeye hakuongea kama mtu wa kawaida, Yeye hakuongea kama Mfarisayo, hakuongea kama kuhani, aliongea kama mtu aliyejua alichokuwa akizungumzia, Naye bila shaka alishawishika na yale aliyosema.

¹³³ “Basi alipomaliza Hotuba Yake, nilisimama na kumtazama kwa mshangao, ndipo akageuka na kuniangalia, Naye akasema, aliniita kwa jina langu, kasema, ‘Jina lako ni Simoni.’ Isitoshe, bali Yeye alijua jina la baba yangu mtauwa, mzee ambaye ametuacha, kasema, ‘Wewe ni mwana wa Yona.’”

¹³⁴ Kasema, “Ndugu, hilo ndilo lililonishawishi ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, Nabii-Mungu, Mungu-Nabii. Nilijua huyo alikuwa ni Masihi, kwa sababu hakuwa na njia ya kunijua, na hata hivyo aliliita jina langu, na baba yangu alisema tumtafute huyo. Isitoshe, bali alinijulisha ya kwamba alijua baba yangu alikuwa ameniambia jambo kama hilo.

¹³⁵ “Siwezi kusahau, ndugu, macho hayo, jinsi yalivyonichoma yaliponiangalia, Naye akasema, ‘Jina lako ni Simoni, na jina la baba yako ni Yona.’” Akasema, “Ulikuwa ni wakati huo ambapo nilishawishika ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi wa Mungu.” Laiti tungekuwa rahisi hivyo alasiri ya leo, laiti ulimwengu ungetambua hilo. “Nilijua Yeye alikuwa ni Masihi.”

¹³⁶ Hapana shaka ilikuwa ni Filipo wakati huo, karibu katikati ya mashua, aliyesema, “Ndugu, ninataka kusimulia juu ya Ndugu Nathanaeli aliyeketi pale kwenye lile kasia lingine.

Nilipoenda kumtafuta, nilishawishika, ndipo nikamsikia akimwita Simoni na kujua ya kwamba jina lake lilikuwa ni Simoni na alijua ya kwamba jina la baba yake lilikuwa Andrea, ama, alijua jina la baba yake lilikuwa ni Yona.” Kisha kasema, “Nilishawishika, kwa hiyo nilitaka kumwona huyu Ndugu Nathanaeli hapa, kwa sababu nilijua alikuwa ni mtu mzuri.

¹³⁷ “Bali nilipoenda kule nikamwambia aje aone Yule tuliyemwona, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu, alisema, ‘Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?’

“Nami nikasema, ‘Njoo uone.’”

¹³⁸ Sasa, hilo ni jambo zuri kufanya, “Njoo ujionee mwenyewe.”

¹³⁹ “Basi tulipokuwa tukienda zetu, unakumbuka ungesema, Ndugu Nathanaeli, jinsi tulivyozungumza, nami nikakwambia wakati ulipowanunua hao samaki kutoka kwa yule mvuvi mzee ambaye hata asingeweza kutia sahihi risiti, asingeweza kuandika jina lake mwenyewe, asiye na elimu kabisa.”

¹⁴⁰ Na hata hivyo, yeye alifanywa kiongozi wa Kanisa na kupewa funguo za kuzimu na mauti, la, zilikuwa funguo za Ufalme, samahani, Yesu alifufuka akiwa na funguo za kuzimu na mauti, alipewa funguo za Ufalme.

Sasa, “‘Naam,’ akasema, ‘ninamkumbuka.’

¹⁴¹ “‘Mbona Yeye alimwambia ya kwamba jina lake lilikuwa Simoni na jina la baba yake lilikuwa Yona. Sasa, wewe ni mtu mwerevu katika Maandiko, hivi Masihi si atakuwa Mtu wa namna hiyo?’

“‘Naam. Naam, hiyo ni kweli.’

“‘Haitanishangaza kama Yeye hakukwambia wewe ni nani, kabla hujaondoka hapo.’

“‘Ah, itanibidi kuliona.’

¹⁴² Ndipo basi wakati Ndugu Nathanaeli alipokuja Mbele za Bwana wetu, Yeye alimwambia, ‘Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake,’ akamshangaza sana.”

¹⁴³ Ndipo Nathanaeli akasema, “Naam, nilishangaa. Nikamwambia, ‘Rabi, uliniona lini Wewe?’

“Naye akasema, ‘Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.’”

¹⁴⁴ “Akasema, “Nilikuwa nimeshawishika kabisa ya kwamba Huyu alikuwa ndiye Masihi, nami nikaanguka kifudufudi mbele ya Mtu huyu, na kusema, ‘Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.’ Nilishawishika, ndugu.”

¹⁴⁵ Andrea, ndugu yake Petro, basi akasema, “Lakini ndugu, sisi sote, siku hiyo, mwajua, wakati alipokuwa akishuka kwenda Yeriko, mwendo wa haraka moja kwa moja hadi Yeriko kutoka Yerusalemu, bali alikuwa na haja ya kupitia Samaria, huko juu kuzunguka kilima, kasema Baba alikuwa akimtuma kwenda

Samaria. Basi tulipofika huko nje, hivi mnakumbuka jinsi miguu Yake ilivyokuwa inauma, Naye alikuwa amechoka na kudhoofika? Naye hata asingeingia mjini, aliketi huko nje karibu na kisima.

¹⁴⁶ “Basi tuliporudi nyuma kisiri, nao wasingeturuhusu kununua chakula, mnakumbuka, kwa hiyo tukarudi kisiri kisimani walipokuwa, ndipo tulipofika kule, tulimwona mwanamke mmoja akija, tukawaza tungesimama tu na kuona kile mwanamke huyu angefanya. Nasi tulijua alikuwa ametiwa alama, mwanamke mwenye sifa mbaya.

¹⁴⁷ “Ndipo alipokuwa akishusha mtungi kisimani, tulisikia mazungumzo yao. Nasi tukamwona Bwana wetu akisimama pale kwa mwanamke huyo, na kuona hizo nywele zikiangukia usoni mwake kwa mshangao wakati Yeye aliposema, ‘Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.’

“Akasema, ‘Bwana, sina mume.’

¹⁴⁸ “Ndipo tukashangaa, ‘Loo-lo! Hapa amekosea kidogo, jambo fulani limetukia sasa.’” Labda kama, kitu kama maskini dada yetu alivyowazia, aliyekuwa ameketi hapa muda mfupi uliopita pamoja na mtoto mchanga. “‘Hapa amekosea kidogo, jambo fulani limetukia sasa, maana Yeye alimwambia aende akamlete mumewe, naye akasema hakuwa na mume yeyote.’” Natumaini maskini huyo mama yuko umbali wa kusikia, mahali fulani. Vema. Yeye ni . . . “‘Hilo hapana shaka lilikuwa ni kukosea kidogo.’”

¹⁴⁹ Na kwa hiyo, akasema, “Vema, sote tulikaa pale vichakani na kusikiliza tuone kile Yeye angesema. Akasema, ‘Vema, sina mume.’

¹⁵⁰ “Akasema, ‘Umesema vema, kwa kuwa umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.’

¹⁵¹ “Iimbadilishaje! Kitambo kidogo, nywele zikaanguka chini, macho yake makubwa, mazuri yakametameta, machozi yakatiririka mashavuni mwake, akasema, ‘Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua ya kwamba Masihi yuaja, na Masihi ajapo, Yeye atatuambia mambo haya.’ Nasi tulishangaa jinsi ambavyo Wasamaria wasio na elimu wangekuwa wakiitazamia ishara ya Masihi, na kujua ishara ya kweli ya Masihi. ‘Tunajua ya kwamba ajapo Masihi. . .’

¹⁵² “Hao watu ambao wasingetupatia chakula kule chini, kuwazia ya kwamba watu hao walikuwa wamefunzwa vizuri vya kutosha kujua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye angetoa ishara ya Masihi.”

“Naam,” kasema, “Sote tulishangaa, mnakumbuka?”

¹⁵³ “Naye akasema, ‘Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.’ Nasi tulikuwa tukilinganisha yale mhubiri aliyosema kumhusu, na yale mwanamke huyu aliyosema kumhusu, mwanamke

mwenye sifa mbaya, hata hivyo alijua zaidi juu ya Maandiko kuliko baadhi ya hao makuhani walivyojua. Walikuwa tu na njia moja wangeweza kusafirira, mwanamke huyu alijua kutokana na dhana ya Kiungu ya Roho.” Kasema, “Angewezaje kujua jambo hilo? Akasema, ‘Ninajua ajapo Masihi, Yeye atatuambia mambo haya. Lakini U Nani Wewe?’

“Akasema, ‘Mimi ninayesema nawe Ndiye.’

¹⁵⁴ “Sasa, sote tulijua wakati huo ya kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi. Tulishawishika. Maandiko yalikuwa yameshuhudia huduma Yake, ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi.”

¹⁵⁵ Ndugu, dada, hivi hamwoni Roho Mtakatifu leo? Roho Mtakatifu hakuacha kushuka wakati aliposhuka kwenye Pentekoste. Usiache mtu yeyote akwambie Roho Mtakatifu ni wa huko nyuma tu. Mtu fulani akijaribu kukwambia uvumi huu wote ambao mmekuwa nao hapa kwa miaka hamsini... Pentekoste ina umri wa miaka hamsini sasa. Miaka miwili iliyopita, nilihubiri ma—mahubiri ya Yubile ya sherehe ya miaka hamsini ya Pentekoste kwenye Hekalu la Angelus. Sasa imekuwa miaka hamsini; mama zenu walikuwa na Roho Mtakatifu.

¹⁵⁶ Pia sikilizeni, kama vile David duPlessis alivyosema wakati mmoja, “Mungu hana wajukuu.” Hiyo ni kweli. Tunapata wajukuu wengi kupita kiasi katika Pentekoste. Hiyo ni kweli. Mungu hana mjukuu, hakuna mahali popote katika Biblia inaposema Mungu ana mjukuu, Mungu ana wana na binti, bali si wajukuu.

¹⁵⁷ Sasa, jambo ni kwamba, sasa ule uamsho wa kwanza wa Kimethodisti, walikuwa wana na binti za Mungu. Ndipo ninii yao... Wao, watu wa kale, wakawaingiza watoto wao, kisha wakawaweka tu katika kanisa la Kimethodisti, hivyo ndivyo hasa Wapentekoste walivyofanya.

¹⁵⁸ Nilihudhuria moja ya makanisa makuu ya Kipentekoste si muda mrefu uliopita, ilikuwa, kwa kweli, yapata miezi mitatu iliyopita, nami nilialikwa kule. Nao walijua jinsi ninavyohubiri utakatifu, basi kila mmoja wa wanawake wao, karibu sana, humo jengoni wamepaka makucha rangi, na wanaume wao wamekata nywele kibapa juu, na chini... Ndipo mara tu shule ya Jumapili ilipokwisha, kila mmoja alitoka kwenye jengo hilo, na kuondoka hapo, walijua watakemewa vikali sana, kwa hiyo kamwe hawakukaa, hivyo tu, hawangekaa na kulivumilia. Hilo halikumsaidia yeyote, kwa sababu itawabidi kukutana nalo kwenye Siku ya Hukumu. Afadhali ukabiliane nalo sasa hivi, na ulimalize wakati kukiwa na rehema. Lakini hapo, hapo ndipo Pentekoste...

¹⁵⁹ Ni kitu gani? Watu wa kale waliokuwa wakiomba usiku kucha, watu wa kale waliokuwa na wokovu halisi, halisi,

wa kweli, waliingia Pentekoste, wakampokea Roho Mtakatifu, wakawaleta watoto wao na kuwaweka kwenye kitanda cha watoto kule chini, ndipo muda si muda mwajua, tuna wajukuu katika Pentekoste. Lakini Mungu hana wajukuu, wote, kila mmoja, wamezaliwa katika Ufalme Wake wana na binti za Mungu. Amina. Wana na binti, si wajukuu, Mungu hana wowote, wote ni wana na binti.

¹⁶⁰ Hiyo ndiyo sababu, siku hizi, Ujumbe huu huwapofusha watu sana ni kwa sababu hawajazoea kuona mambo ya kimbinguni, tunahitaji nguvu za Mungu, tunahitaji kurudi kwenye Pentekoste halisi. Kama Billy Graham alivyosema hivi majuzi, “Huwezi kulipuuza kanisa la Kipentekoste, kwa sababu ndilo kanisa linalopanuka upesi kuliko yote ulimwenguni siku hizi.”

¹⁶¹ *Mgeni Wa Jumapili* la kanisa Katoliki lilisema mwaka jana kwamba kanisa la Kipentekoste liliandikisha waongofu milioni moja, laki tano katika mwaka mmoja, ambapo kanisa Katoliki, lenyewe, halikuandikisha nusu ya hiyo.

¹⁶² Huwezi kulipuuza pamoja na wahudumu wote mashuhuri kote nchini, kanisa la Kipentekoste bado linachukua nafasi za mbele. Kwa nini? Huwezi kulikomesha. Hiyo ni kweli. Mungu aliliagiza, nalo limeondoka. Lakini linapofikia mahali, linaanza kuwaingiza wajukuu, likichukua, na kuokota mambo ya ulimwengu, Mungu ataendelea moja kwa moja, kutakuwa na kundi lingine litakalolichukua, na kuendelea moja kwa moja. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo rudi kwenye mstari wa mbele wa vita, ndugu. Kaa chini ya upako, usiache chochote kikusumbue.

¹⁶³ Sasa, turudi kwenye ishara hizo, leo, tunapoishi katika siku ya mwisho, tunapona ya kwamba kule kufunikwa kwa ile piramidi, lile jiwe lililokataliwa kutoka kwenye ile piramidi, kamwe hawakupata kujua ni kwa nini lile—lile jiwe la pembeni lilikataliwa hekaluni. Lakini hawawezi kupata jiwe ambalo lingepatoshea. Lakini sasa, linapoanza kulundikana juu, kila moja ya hayo mawe yakitoka kwa Luther, Methodist, Pentekoste, basi itabidi Kanisa lifikie mahali ambapo lile Jiwe halisi la Kuwekwa Juu litakapokuja, Litashikamana moja kwa moja pamoja Nalo, kama nilivyosema jana usiku juu ya lile agano.

¹⁶⁴ Itabidi Kanisa liwe na Roho wa Mungu ndani Yake sana, mpaka Roho huyo atakuwa akifanya kazi zile zile ambazo Yesu Kristo alifanya hapa duniani, Roho Mtakatifu akiwa na mamlaka kamili kabla ya Mwanamke huyo, lile Kanisa, kuweza kuungana na Mumewe, Bibi-arusi.

¹⁶⁵ Wajukuu kamwe hawataona jambo hilo, wanasema tu, “Mimi ni Mpentekoste, hivyo tu,” wanaendelea. Pentekoste si dhehebu, Pentekoste ni tukio ambalo mtu yeyote anaweza kupata, ni Kanisa lililoitwa litoke, Kundi lililoteuliwa, dogo.

¹⁶⁶ Angalieni katika siku za Sodoma kama tulivyohubiri juma hili, kulikuwa na wale wahubiri mashuhuri walioingia Sodoma na kuanza kuhubiri, walihubiri Ujumbe kule chini. Lakini Mmoja alibaki nyuma na kufanya ishara katika Kanisa hili dogo katika uchache. Angalieni ishara alizofanya, naye Yesu alisema jambo lilo hilo lingejirudia kwa Mataifa katika siku hii ya mwisho, nalo hili hapa.

¹⁶⁷ Sasa angalieni, kunachelewa, loo, giza lilikuwa karibu kuingia, nao walikuwa wakizungumza, nao wakaendelea, kasema, “Afadhali tupige makasia, ndugu.”

¹⁶⁸ Ndipo ikatokea Shetani aliangalia chini kutoka juu ya lundo la moshi, ikatokea yeye aliangalia, naye akaona hao wanafunzi walikuwa wameondoka bila Yesu, kasema, “Hii hapa nafasi yangu.”

¹⁶⁹ Ndugu, mengi sana ya hayo yatalingana na siku hizi, kanisa linajaribu kuendelea bila Yesu. Tumekuwa na saa ya ufanisi wakati watu walipopata mishahara mikubwa, muungano, na kadhalika namna hiyo, wakipata pesa nyingi, watu maskini wanazo. Imeingia miongoni mwa Wapentekoste, mpaka kuna mamilionea, na kila kitu katika Pentekoste, ambalo ni sawa. Sisi...Ni kwa ajili ya...Si sana kwa wasiojiweza, ni kwa matajiri, pia, Mungu ni kwa ajili ya wote, matajiri au maskini, kila mtu. Kutakuwako na yakara wengi kuzimuni kadiri kutakavyokuwako na mamilionea.

¹⁷⁰ Ni mtazamo wako kuhusu yale Mungu aliyokupa. Je, uko tayari kutumia pesa zako kwa ajili ya Ufalme wa Mungu? Kama ndivyo, Mungu atakubariki, kama ni senti moja, ama kama ni kama zile yule msichana mdogo alizonipa jana usiku, ama—ama milionea fulani mashuhuri mwenye thamani ya dola milioni nyingi, ni mamoja tu kwa Mungu.

¹⁷¹ Sasa, tumekuwa na wakati wa ufanisi, tumekuwa na majengo makubwa, na kujenga makanisa makubwa na viti vizuri tukajenga shule kubwa kubwa, na kadhalika, mpaka ninahofia kwamba tunaondoka bila Yesu, ibilisi anaona jambo hilo.

¹⁷² Naye akawaona bila Yesu, kwa hiyo akaanza kupuliza pumzi yake, “*Whiu!*” akileta upepo, kasema, “Sasa ni wakati wa kuwaondoa, wako huko nje peke yao, yeye hayuko pamoja nao, kwa hiyo tutaninii tu...Nitapulizia tu pumzi yangu juu yao, na hiyo itafanya kazi. Tutawazamisha moja kwa moja huko nje baharini, nasi tutawaondolea mbali.”

¹⁷³ Ndipo alipoanza kupuliza pumzi yake ya sumu, meli ikaanza kuyumbayumba huku na huku, makasia yakavunjika, matanga yakaanguka, nayo maskini meli hiyo ilikuwa inajaa maji. Matumaini yote kwamba wangeweza kuokolewa yalikuwa yametoweka.

¹⁷⁴ Na karibu iko hivyo sasa, enyi marafiki. Angalieni hapa, angalieni mjini leo, angalieni miamsho, angalieni mahali mahali,

kila kitu, tuna pesa nyingi sana, inatubidi kuchukua mamilioni ya dola na maelfu ya dola kwa juma, nasi hatuna budi kufanya *haya yote, yale, na mengineyo*, na mipango ya namna *hii*, na *ile*.

¹⁷⁵ Tumelipanga sana, hata hakuna wakati wa mkutano wa maombi, mahubiri ya dakika ishirini, ama *chochote kile*, hata imefikia mahali, hata wavulana wengi wasomi wenye elimu wakaingia, mpaka hapa si muda mrefu uliopita, niliingia kwenye ka—kanisa kuu la Kipentekoste kuwaomba kama ningeweza kuazima viti niingie kwenye jumba langu la mikutano mahali nilipokuwa, naye mchungaji akasema, “Nisingemruhusu mtu yeyote kuketi kwenye viti vyangu ambaye hata anaamini katika uponyaji wa Kiungu.” Hiyo ni kweli, Hot Springs, Arkansas.

¹⁷⁶ Sasa, halafu basi, kana kwamba imefikia mahali, na mengi ya makanisa makubwa yanayojaribu kuzima kitu hicho, wakisema tunatilia mkazo sana uponyaji wa Kiungu, juu ya mambo haya mengine, na kuyafanya tu taratibu za dini. Ni kitu gani? Mnawaingiza wajukuu ndani yake, mnaingiza wasomi ndani yake, badala ya watu waliookolewa na Mungu.

¹⁷⁷ Kila mtu anayeingia jukwaani hana budi kuwa ni maskini *Hollywood*, mrembo, mwenye nywele za mawimbi. Tuna uinjilisti mwingi sana wa *Hollywood* siku hizi, wahubiri huko nje jukwaani, nao wake zao wakitembea huku na huko kana kwamba wamemwagwa kwenye sketi, wamejaa vito mikononi mwao, na rangi ya midomo, na nywele fupi. Mbona, ni fedheha kwa ulimwengu! Na kuiita Pentekoste. Huenda ikawa ni Pentekoste kwa madhehebu, si Pentekoste kwa tukio. Hiyo ni kweli. Tunahitaji Pentekoste ya mtindo wa kale, ya Roho Mtakatifu tena.

¹⁷⁸ Ibilisi alituona tukienda kombo kwa majengo makubwa, na madhehebu makubwa, na *hili* kuu, na *lile* kuu, na kumwacha Yesu nje. Naye ibilisi ameanza kupuliza pumzi yake ya sumu akisema, “Vema, tunapanda juu sasa. Tunaendelea vizuri zaidi siku hizi, nasi tuna kundi bora zaidi la wahubiri, wenye akili, watu waliovalia nadhifu, mambo haya yote mbalimbali.”

¹⁷⁹ Ninapenda... Na kuimba? Nilienda mahali fulani hapa hivi majuzi ambapo walikuwa na kwaya ilikuwa iimbe kabla tu sijawaomba wagonjwa na kuhubiri. Basi kwaya hii kuu ya Kipentekoste, ikisimama kule nyuma, naye huyo mtu alikuwa anaenda kuchukua sadaka, na kama hawakuikufuru, kuidhihaki, wakifanya mizaha, wakitania huku na huku, mmoja kwa mwingine. Kundi la wanawake waliojipaka rangi ya midomo na poda nyekundu, na hizo nyusi zote zikionekana kitu kama ibilisi, zote zimeng’olewa ila mchirizi mmoja mdogo wa mti wa kiberiti usoni mwao, na vitu kama hivyo, wamesimama pale.

¹⁸⁰ Loo, kama hawangalinitupa nje! Nilitembea huku na huku sakafuni nikisema, “Mungu nishikilie, nifunge tu mdomo wangu,

tafadhali mpaka nitakapomaliza mkutano huu.” Niliwazia ningetembea huko nje, na kusema, “Hustahili kuimba katika kwaya kwa ajili ya Ufalme wa Mungu!”

¹⁸¹ Wamevaa majoho, hilo ni sawa, majoho ni sawa, hilo ni sawa, ila haikuwa hayo, bali ni ile roho iliyo mle chini. Wakasimama huko nje na kujaribu kuimba namna fulani ya . . . mimi. . .

¹⁸² Kama kuna chochote, nikipendacho ni uimbaji mzuri, wa mtindo wa kale, wa Kipentekoste, ambapo kama mtu hana hata sauti ya kuwaita nguruwe, ataitumia kwa utukufu wa Mungu na kuimba katika Roho. Ninachukia sauti iliyofunzwa kupita kiasi inayoshikilia juu kule namna fulani ya tuni mpaka wanageuka bluu usoni, “*Ahhh!*” Hata wao wenyewe hawajui wanalosema. Roho Mtakatifu anawezaje kuingia katika kitu kama hicho? Siupendi huo. Ninapenda uimbaji wa kweli, wa Roho Mtakatifu, ambapo wanaimba na kupiga makofi na kumsifu Mungu.

¹⁸³ Kuna nini? Ibilisi anapulizia pumzi yake ya sumu, kasema, “Mnataka kutenda kama hao wengine.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁸⁴ Yesu hakuwa amewaacha. Mlisikia mahubiri yangu juu ya mwana-kondoo na hua, wakati hua aliporuka, alipomrukia mbwa mwitu, yeye si mwana-kondoo. Sasa, Yesu hakuwa amewaacha. Yeye alifanya nini? Alipanda juu ya mlima mrefu sana uliokuwepo, kusudi aweze kuwaangalia kote baharini. Naye alipowaona katika shida, alikuja kwao akitembea juu ya bahari.

¹⁸⁵ Hajatuacha, anathibitisha hilo sasa, hajatuacha. Hakupanda mlima mrefu kuliko yote, alipanda Kalvari, akaendelea kupanda mpaka akaja Mbele za Mungu kwenye Kiti cha Enzi Utukufuni. Alipanda juu sana, angeweza kuona ulimwengu kutoka kwenye Kiti Chake kikuu cha Enzi. “Jicho Lake linawaangalia shorewanda, nami ninajua Yeye ananiangalia,” Yeye anakuangalia. Anaungalia mkutano huu, anataka kuona matokeo yake yatakuwaje. Atakuja kunena, afanye ishara na maajabu, kisha aondoke na moyo uliovunjika, kwa sababu watu wanamkataa.

¹⁸⁶ Angalieni, huyu hapa anakuja usiku wa manane, wakati matumaini yote yamekwisha, makasia yakavunjika, meli ikajaa maji, walikuwa wanashikana na kupiga mayowe. Waliona nini? Walimwona Yeye akija, akitembea juu ya bahari. Nao walipomwona, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia, walikiogopa, wakasema, “Ni mzuka. Kuna jambo fulani la kigeni kuhusu hilo, kinatisha.” Na kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia walidhani kilikuwa ni mzimu.

¹⁸⁷ Na hivyo ndivyo ilivyo na ulimwengu siku hizi. Wakati mabomu ya atomiki nchini Urusi, na makombora ya kila namna na kadhalika yananing’inia kwenye mabanda ya ndege, UN inazama, na mataifa yote yanapingana, na yote tunayofanya ni

kujaribu kununua ushirika na urafiki. Huwezi kununua ushirika na urafiki, haina budi kuwa ni karama ya Mungu kufanya hivyo, bila shaka. Kama vile ndoa iliyojengwa juu ya kitu kama hicho kamwe haitadumu. Sikilizeni, enyi marafiki, hamwezi kufanya hivyo.

¹⁸⁸ Na katika saa hiyo yenye giza, Kitu pekee ambacho kingeweza kuwasaidia kiliwajia, nao wakakiogopa, ndivyo ilivyo leo. Leo hii Roho Mtakatifu anakuja miongoni mwetu, katika makanisa yetu, nao ulimwengu wa nje unaangalia pande zote, na kusema, “Loo, hiyo ni telepathia ya kiakili. Ah, ah! Huo—huo ni upiga ramli. Hiyo ni . . .” Kitu chenyewe na Kitu cha pekee kinachoweza kuwasaidia, wanakiogopa.

¹⁸⁹ Naye Yesu, kwa somo langu, alisema, “Msiogope; Ni Mimi. Msiogope; Ni Mimi.”

“Unajuaje ni Yeye?”

¹⁹⁰ Kwa sababu hufanya kazi Zake. “Kwa tunda lao mtawatambua,” kwa tunda la Roho, mnaona yale wanayofanya, mnaona kazi ambazo Yesu alifanya. “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.”

¹⁹¹ Sasa, shida yake ni kwamba, tunachukua jambo moja dogo katika Biblia. Wamethodisti, wana utakaso, wangelidumu moja kwa moja nao, wasingeyumbayumba hata kidogo; Luther alipata kuhesabiwa haki; Wapentekoste walipata Roho Mtakatifu, wakinena kwa lugha, hivyo ndivyo tu wanavyofanya.

¹⁹² Sasa, kumbukeni Biblia imejaa ahadi za Kiungu, Mafarisayo walikuwa na njia yao kulihusu. Lakini wakati Yesu alipokuja, Yeye kamwe hakupinga Maandiko, alikuja jinsi hasa Maandiko yalivyosema, bali walidhani Yeye alikuwa anakuja kwa njia nyingine. Ilibidi aje jinsi walivyoliwazia, hilo ndilo jambo lile lile lililotukia leo.

¹⁹³ Tumeingia katika madoido, tuone kama tunaweza kupata wengi zaidi katika dhehebu letu, kusema maovu dhidi ya huyo mwingine, kumrarulia mbali kujenga letu, kubadilisha dini, na, “Milioni moja zaidi katika mwaka wa ’44,” kama Baptisti ilivyosema katika mwaka huo. Haya basi. Wanapata nini, ila wanaojiunga na kanisa? Wakati uo huo iliwabidi kuliruhusu kanisa liondoke, na kutoa dakika kumi na tano kusudi watu wote pamoja na mchungaji wasimame uani na kuvuta sigara kabla hawajarudi ndani tena. Msiniambie, nilikuwa mumo humo kwenye kanisa la Kibaptisti wakati lilipotukia. Kwa hiyo haya basi.

¹⁹⁴ Hilo lina faida gani? Tunachohitaji leo hii ni Injili safi, ya Kipentekoste pamoja na nguvu za Roho Mtakatifu kurudi kanisani tena. Biblia imejaa ahadi, ndugu yangu, kuna ahadi nyingi *hapa* ndani kwa ajili yako.

¹⁹⁵ Kama tu hivi majuzi, kulikuwako na mwa—mwanamke ambaye alikuwa maskini sana hata ninii, walimchunguza huyo mwanamke mkongwe wapate kujua, shirika la kutoa misaada lilifanya hivyo, waone kile wangeweza kumfanyia. Walipanda huko na kusema, “Una umri gani?”

Naye akasema, “Nina umri wa miaka themanini.”

Kasema, “Nawe ni fukara.”

¹⁹⁶ “Naam.” Hata hakuwa na chakula, alikuwa hana chakula, alikuwa ameuza fenicha zote za nyumba. Naye alikuwa... Baadhi ya majirani wakazirudisha. Alikuwa na kiburi kidogo juu yake, na kwa hiyo asinge—asingesikiliza, ndipo hatimaye, akaona ilimbidi awe nazo.

Kwa hiyo wakamwambia ya kwamba... “Vema,” akasema huyo mpelelezi alimwambia, kasema, “mama, una watoto wowote?”

Kasema, “Ndiyo, ninaye mwana mmoja.”

Kasema, “Yuko wapi?”

Kasema, “Yuko India.”

“Ati India?”

“Naam.”

Kasema, “Anafanya nini kule?”

Anasema, “Yeye ni mfanyabiashara.”

“Vema,” kasema, “Kwa nini usimwache akusaidie?”

¹⁹⁷ Akasema, “Unajua nini? Yeye ni mvulana mpendwa, mzuri sana,” kasema, “yeye huniandikia barua nzuri kuliko zote ulizowahi kuona.” Kisha akasema basi, “Lakini siwezi kuwa na ujasiri wa kumwomba, hiyo ndiyo sababu nisingeweza kuwaomba ninyi nyote. Nisingeweza kumwomba mvulana wangu wa thamani, yeye anajua hali yangu, naye anajua ya kwamba ninahitaji pesa, na kama angekuwa na pesa, angenitumia. Kwa hiyo, siwezi kwenda kumsihi mwanangu afanye hivyo.”

Ndipo kasema, “Yeye huandika,” kasema, “hukuandikia?”

¹⁹⁸ Kasema, “Yeye huniandikia angalau mara moja kwa mwezi, mara kwa mara tu,” kasema, “wakati mwingine mara mbili.” Kisha kasema, “Mimi hupata picha nzuri sana kutoka kwake, yeye daima hunitumia picha. Nami nafikiri hizo ni za kupendeza sana, daima ninazifurahia sana.”

Kasema, “Ni picha za aina gani?”

Kasema, “Loo, nitakuonyesha.”

Kasema, “Unazo?”

Kasema, “Ndiyo.”

Kasema, “Ziko wapi?”

Akasema, “Ziko katika Biblia yangu.”

¹⁹⁹ Basi akaiendea Biblia yake, na kuanza kuzitoa. Mnajua zilikuwa nini? Hawala za fedha za India. Alikuwa na makumi ya melfu ya dola katika hawala za fedha za India bila kujua zilikuwa ni nini, kwa sababu zilikuwa zimejaa picha za kupendeza, naye alidhania zilikuwa ni picha tu.

²⁰⁰ Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, enyi marafiki, Biblia hii ya kale imejaa tu hazina, kote kule. Kwa nini uwe mgonjwa au fukara? Kwa nini uwe baridi na asiyejali, wakati Biblia imejaa ahadi za Mungu? Msiogope, ni Bwana Yesu. Mnaamini hilo?

²⁰¹ Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Sikufikia mahali nilipotaka kufikia, lakini kunachelewa, nanyi mna ibada za jioni. Na tuombe sasa.

²⁰² Baba yetu wa Mbinguni, kweli, Biblia imejaa ahadi, na kila ahadi ni halisi, kila ahadi ni yetu. Ulikufa kusudi ahadi hizi zipate kutimizwa ndani yetu. Jalia watu wasiogope wanapoona jambo hilo ulilonena kwamba lingetimia, wakiliona likitendeka moja kwa moja miongoni mwao.

²⁰³ Jalia walikumbatie, na kusema, “Naam, Yesu, karibu kwenye mashua yangu ndogo, inarushwa-rushwa huku na huku. Daktari aliniambia nilikuwa na kansa. Daktari aliniambia nilikuwa na uvimbe. Daktari aliniambia nilikuwa ninaingia upofu. Daktari aliniambia nilikuwa na TB, magonjwa haya yote. Maskini mashua ndogo inajiandaa kuzama wakati ikisafiri kwenye barabara kuu ya maisha.”

²⁰⁴ Sasa, jalia wasiogope, alasiri ya leo, watakapokuona Wewe ukishuka kupitia kwenye ushoroba wa Utukufuni, ukishuka kuingia katikati ya watu. Jalia waseme, “Naam, Bwana, hatuogopi, bali tuko hapa sasa tukikuamini Wewe.” Na jalia wakukaribishe ndani kama wanafunzi walivyofanya; na mara hiyo dhoruba ikakoma, nao walikuwa ufukoni.

²⁰⁵ Mungu jalia, alasiri ya leo, kwamba watu wengi hapa watakaokuona ukitembea miongoni mwa watu leo, tunapowaombea, jalia watambue na kuamini kwa mioyo yao yote, na twaomba Wewe uje moyoni mwao, na jalia wakupe nafasi, na kukukaribisha katika maskini chombo chao cha magonjwa au dhambi, na yote yatatatuliwa. Tujalie, Baba.

²⁰⁶ Sasa, huku tumeinamisha vichwa vyetu, kuna mtu hapa ndani usiyemjua Yesu kama Mwokozi wako? Kabla jambo lolote halijatukia, ungesema, “Ninataka kumkubali kama Mwokozi wangu binafsi.” Inua mkono wako kama unataka kumpata Kristo kama Mwokozi wako binafsi. Waweza kuinua mkono wako? Kunaye hata mmoja? Ninakuuliza, wewe ndiye hakimumu, unaijua nafsi yako.

²⁰⁷ Kuna mmoja humu ndani ambaye amerudi nyuma, angetaka kumrudia Kristo? Mtu anayetaka Uzima wa Milele angetaka

kuja? Mimbara imesimama hapa, madhabahu iko wazi, nasi tuko papa hapa kutanguliza mambo ya kwanza: Ufalme wa Mungu. Tuko papa hapa kuomba pamoja nawe, mpaka Mungu atakapoitakasa nafsi yako na kukujaza na Roho Mtakatifu. Kama utainua tu mkono wako, na uje mbele sasa, tutafurahi kukupokea.

²⁰⁸ Haidhuru kuna joto jinsi gani, endapo hauko sawa na Mungu, utaingia mahali pa joto kuliko hapa. Kwa hiyo wewe—wewe njoo sasa na uwe tayari kumpokea Bwana Yesu. Kama uko hapa, tunakungojea.

²⁰⁹ Tunapongojea kidogo tu huku vichwa vyetu vimeinamishwa, hebu tuuvumishe wimbo huu, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kila mtu aombe, nanyi Wakristo wote ombeni, huenda kukawa na mwenye dhambi hapa mwoga kidogo. Sasa, nitasubiri kidogo, ili kwamba sitawajibikia hali yao ya kupotea kwenye Siku ya Hukumu. Tunapovumisha sasa:

“Karibu nimeshawishika,” sasa kuamini;
 “Karibu nimeshawishika,” Kristo kumpokea;
 Inaonekana sasa . . . “ . . . Roho . . . Njia yako;
 Siku iliyo rahisi zaidi, nitakuita Wewe.”

Mara moja tu zaidi tafadhali.

. . . mavuno yamepita!
 “Karibu nimeshawishika,” maangamizi
 yanakuja hatimaye!
 “Karibu . . .”; “Karibu” ni . . . kushindwa!
 Inasikitisha, inasikitisha, kwamba
 uchungu . . .

Ninasimama nikingojea. Roho Mtakatifu anangojea. Utakuja?

. . . “Karibu—lakini nimepotea!”

²¹⁰ Baba wa Mbinguni, kama kuna wale hapa, Bwana, labda huenda wamedanganyika, labda Shetani anawaambia ya kwamba wako tayari wakati hawako tayari, “Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu.” Kama hiyo . . . Natumaini hawapo, Baba, lakini kama wapo, ninaomba ya kwamba utawashawishi, Baba. Ninaomba ya kwamba waliketi hapa kwenye chumba hiki chenye joto alasiri ya leo kunisikiliza nikiupitia ujumbe huu, Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawaokoa. Tujalie.

²¹¹ Jalia jambo fulani lifanyiike baadaye kidogo katika ibada ambalo litawafanya waamini, kwa uponyaji wa wagonjwa ama wanaoteseka, ama kitu fulani. Jalia kwamba jambo fulani lifanyiike kuwashawishi waje Kwako. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

²¹² Sasa, kwa saa ya ukutani pale, ni saa kumi na dakika ishirini. Sasa, tunataka tuwe tumetoka katika muda mfupi tu. Nilimtuma

mwanangu na hao wengine (Ama, hivi uligawa kadi, ama Billy? Billy?), vema, kugawa kadi za maombi. Uligawa zipi? E? D? D, moja hadi mia moja? Vema. D, moja hadi mia moja, tuliwaambia watu wote jana usiku, wote wanaotaka kuombewa. . .

²¹³ Sasa, katika mstari huu, katika mstari huu, tutawaombea watu kulingana na vile ambavyo Ro—Roho Mtakatifu amenipa kuwaombea watu.

²¹⁴ Sasa, namba moja, ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? Waweza kuinua mkono wako? Je, mama huyo anaweza kuja asimame papa hapa? Wakati akija, namba mbili, utakuja? Namba mbili, kadi ya maombi D, namba mbili. Vema, mama. Namba tatu, waweza kuinua mkono wako? Namba tatu. Mnaona, baadhi yao itatubidi kuwabeba. Vema, namba tatu. Namba nne. Namba nne waweza kuinua mkono wako? D, kadi ya maombi D, kama katika Duncan. Mnaona? D, namba nne. Vema, njoo, mama.

²¹⁵ Namba tano, namba tano. Upesi, namba tano. Huna kadi ya maombi tena, siyo mama? Kuna mmoja wenu nyote aliye na kadi ya maombi hapo? Mama uliye—uliye kitini, una kadi ya maombi? Sawa. Sasa, namba tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. Mimi—mimi. . .

²¹⁶ Huu ndio mkutano pekee niliowahi kuwa nao maishani mwangu, hata hivyo, ambao nisingeweza kuwafanya watu wenye kadi ya maombi waje huku na kuombewa. Namba. . . Kwa kawaida, wanachaniana, lakini, kwa namna fulani, haininii tu. . . haijafanya kazi hapa. Tumekuwa na hiyo. . . Ni wangapi wanaojua hilo? Tumekuwa nalo usiku baada ya usiku, tunawaita, hata wasingekuja.

²¹⁷ Vema. D, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, hebu waje. Kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, na waje. Nimepata mmoja, wawili, kutoka kwa hizo. Kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini. Mtu fulani anachukua kadi na kuondoka humu jengoni, mnaona, anaondoka, na hilo ndilo linalolisababisha.

²¹⁸ Ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano. Ishirini na sita, ishirini na saba, ishirini na nane, ishirini na tisa, thelathini. Thelathini na moja, thelathini na mbili, thelathini na tatu, thelathini na nne, thelathini na tano.

²¹⁹ Sasa, mnaona, watu wanachukua kadi na kuondoka. Usininii. . . Hawapaswi kufanya hivyo. Kama ukipata kadi, unapaswa kubaki tu, unapaswa kubaki humu—humu jengoni. Thelathini na tano, thelathini na sita, thelathini na saba, thelathini na nane, thelathini na tisa, arobaini. Hilo ni sawa, sasa tunafikia mahali fulani. Arobaini, arobaini hadi hamsini, hebu wasimame. Wote mlio na kadi ya maombi D, simameni hapa. Nafikiri hizo ndizo zote zilizosambazwa.

²²⁰ Je, kulikuwa na kadi zingine zilizotolewa, Billy, mbali na D? Gene? Gene? D tu, D tu. Vema. Kila mtu awe na kicho sana basi. Sasa, kadi ya maombi namba D, simama, hizo ndizo kadi za maombi. Vema, wote walio na kadi ya maombi D, hata kufikia mia moja, simameni.

²²¹ Kuna mtu yeyote hapa ndani ambaye ni mgonjwa ambaye hana kadi ya maombi, aliyekuja amechelewa sana kupata moja? Inua mkono wako. Mbili au tatu, nne, tano, sita, saba. Vema, hebu kidogo. Tunawaombea hawa kwanza, halafu wewe . . . ndipo tuta—tutaona kama tunaweza kuwaingiza humo, pia.

²²² Vema. Sasa, jambo fulani halina budi kutukia sasa, sivyo? Sasa, ni wangapi wanaoamini sasa, kwa kuwa nimewaambia huduma mbalimbali, ya kwamba awamu hii ya mwisho ya huduma itakuwa kubwa kuliko zingine? Hakika, itakuwa. Itaachwa juu ya watu, bali itakuwa kweli halisi, kwa njia hii Roho Mtakatifu anaweza kufunua na kusema mambo mbalimbali; lakini haitaponya, haiwezi kuponya.

²²³ Hebu warudi nyuma kidogo huko nje, enyi wavulana. Msiwaache wasimame katika . . . waende kwenye jua, acheni tu—acheni wasimame papo hapo, ili waweze kuingia moja kwa moja kwenye mstari wa maombi, waingie moja kwa moja. Sawa.

²²⁴ Hivi mlishangaa ni kwa nini tunapowapitisha tu mstarini, kuwaombea, tunawapa kadi ya maombi? Ni wangapi wangetaka kujua ni kwa nini? Mngetaka? Kuwazuia wasirudi mstarini tena. Wa—watarudi moja kwa moja. Nimeona—nimeona watu wakienda, wakipitia mstarini mara tano, wakiendelea tu kuzunguka, tena, na tena. Na kila unapoenda, inakudhoofisha zaidi kiasi hicho, kiasi hicho zaidi, kiasi hicho zaidi.

²²⁵ Wanapewa tu kadi ya maombi, kwa hiyo, wanapokuja jukwaani, hawana budi kushikilia kadi yao ya maombi mkononi mwao, mtu fulani anachukua hiyo kadi ya maombi, na kuwapitisha tu mstarini. Mnaona? Na hiyo ni kuwazuia wasirudi tena. Ni kwa manufaa ya watu. Mnaona? Wao . . .

²²⁶ Unaona, lazima mkumbuke, ya kwamba katika mwanadamu, hakuna kitu kinachoweza kukusaidia. Ni wangapi wanaojua hilo? Hakuna kitu ndani ya mwanadamu. Tuna watu mashuhuri nchini leo, tunaye Ndugu Roberts, Ndugu Tommy Osborn, Ndugu Freeman, Ndugu Allen, watu mashuhuri wa Injili, lakini hata hivyo, hakuna kitu kimoja katika yeyote wa watu hao kinachoweza kukuponya. Kama mtu yeyote akisema hivyo, bila shaka yuko nje ya mwelekeo wa Maandiko, kwa kuwa “Yesu *alijeruhiwa* kwa makosa yetu, kwa kupigwa *Kwake, tuliponywa*.” Ni wangapi wanaamini hilo?

²²⁷ Hiyo ndiyo sababu nilitofautiana na ndugu huyo si muda mrefu uliopita. Nanyi nyote mnayo hapa nje, ilienea kote katika nchi hii, ile “Mpendwa Ndugu Branham.” Hiyo ilitokea

kuwa si yule mtu aliyesema waliandika, ilikuwa ni mtu mwingine. Ilionekana kana kwamba mtu huyo angalijua ningelijua hilo. Najua ni nani aliyeandika hiyo barua, nilijua kabla haijaandikwa kwamba itaandikwa. Sasa, Mungu anajua hilo. Nilijua itaandikwa.

228 Kuhusu damu mkononi kuwa ni ushahidi wa Roho Mtakatifu, wakimchukua mwanamke fulani kutoka India na kumleta. . . Yeye ni *Madonna*; tuna mmoja nyumbani, yeye ni Mkatoliki, kahaba, mlevi sugu, kila siku ishirini na nane, amejaa damu mikononi, amejaa damu miguuni, amejaa damu kwenye paji la uso.

229 Jamaa huyu akaniambia, mhubiri huyu mashuhuri, kasema, “Lakini Ndugu Branham, kila wakati Roho Mtakatifu anapokuja juu ya mwanamke huyu, mbona jambo hili hutukia.”

230 Nikasema, “Naam, kila wakati mwanamke *huyu* anaposisimkwa, linatukia, pia.”

231 Kama damu hiyo itawaokoa watu, ilikuwaje kwa Damu ya Yesu? Imeondolewa. Ni upinga-Kristo. Hakuna kitu kama hicho. Usifanye kitu kama hicho, huo ni upinga-Kristo. Sasa, kile watu wanachoamini kuhusu miamsho midogo, acha waendelea na kuliadini, lakini wakati wowote anapokuja, ukiondoa, ama, ukileta roho ya mpinga-Kristo katika kanisa la Kipentekoste, ni kazi yangu kupingana nalo. Hiyo ni kweli. Sio dhidi ya huyo mtu, bali dhidi ya roho anayeingiza humo ndani. Hiyo ni kweli.

232 Wanawake, kama vile, mafuta yakitiririka mgongoni mwao, wakiyaweka kwenye kitu kidogo, na kuwapelekea watu wapate kuponywa. Mbona, kama mafuta yatawaponya watu, vipi kuhusu Damu ya Yesu ambayo. . . ? Nini. . . ? Hiyo imeondolewa Kwake. Damu chafu ya ki—kitu cha siku ishirini na nane pamoja na mwanamke ingeweza kuokoa nafsi, wakati ile Damu ya thamani ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliyezaliwa na bikira, ilimwagwa pale Kalvari? Inanibidi tu kupinga jambo hilo, mimi, kuna jambo fulani tu kulihusu, inanibidi tu kufanya hivyo, mnaona. Ni makosa! Ni makosa!

233 Sasa, ukitaka kusema, “Nilimpata Roho Mtakatifu nikisimama kwa kichwa changu.”

234 Amina, endelea, sijali ulichopata.

235 Unasema, “Nilimpata kwa kuona nuru kubwa.”

236 Endelea na uone nuru kubwa. Amina. Kama ukiishi hayo maisha, ninaamini ulimpata.

237 Unasema, “Nilimpata nikinena kwa lugha.”

238 Amina. Kama ukiishi hayo maisha, ninaamini unaye; kama huyaishi hayo maisha, hukumpata, hivyo tu. Unaona?

239 Huna budi kuwa na huo Uzima huko nyuma, “Kwa matunda yao, mtawatambua.” Hiyo ni kweli. Ninaamini katika kunena

kwa lugha, ninaamini katika kupaza sauti, ninaamini katika matukio yote ya Kipentekoste, naam, lakini kama halijaninii... kama hilo halijafungwa pamoja na upendo, halitafanikiwa kamwe. Upendo ndio unaolitimiza.

²⁴⁰ Wakati yule fahali alipokuwa akitaka kuniua siku ile, alinjia mbio moja kwa moja... Wakati huyu mwendawazimu... Loo, kuna mambo mengi sana. Kama ni... Sikumkasirikia mtu huyo, niliwazia, "Maskini jamaa huyo! Hataki kunidhuru, huyo ni ibilisi ndani ya mtu huyo." Ni wangapi walikuwako wakati jambo hilo lilipotukia? Nami nikasema... Hakika. Nikasema, "Kuna..." Sikumdharau. Nilisema...

Akasema, "Usiku wa leo nitakurusha katikati ya kusanyiko hilo."

²⁴¹ Angeweza kufanya hivyo, pia. Alikuwa na yapata ratili mia mbili ama mia tatu, mrefu *hivyo*, nami nilikuwa na uzito wa mia moja ishirini na nane, alikuwa na uwezo wa kimwili. Sikutaka... kamwe sikusema kitu, ngoja. Niliacha tu Roho Mtakatifu aliseme. Ndipo akasema yale atakayofanya.

²⁴² Ndipo Roho Mtakatifu akajibu, "Kwa sababu ulimpa changamoto Roho wa Mungu, usiku wa leo utaanguka miguuni pangu."

Akasema, "Nitakuonyesha nitaanguka kwenye miguu ya nani," akaurudisha nyuma mkono huo mkubwa.

Nikasema, "Toka ndani yake, Shetani."

²⁴³ Ndipo macho yake yakatokeza nje kabisa namna hiyo, akavimba namna *hiyo*, akaanguka chini, na kuibana miguu yangu sakafuni.

²⁴⁴ Ikaonyesha Mungu wa Daudi angali hai. Bila shaka. Anaweza kumshinda Goliathi kwa misingi yoyote atakayokutana naye. Lakini afadhali usijaribu kulifanya wewe mwenyewe, afadhali umwache Roho Mtakatifu aliseme, maana mnaona, huduma yote ya miaka hii imefanya kazi kufanikisha huduma hii mpya sasa, kuirudisha nyuma, "Kama unaweza kuamini. Ninaweza kama utaamini." Mnaona? Loo, itakuwa ajabu, nina hakika tu, vema, kama unaweza kuamini.

²⁴⁵ Sasa, ni wangapi walio humu jengoni ambao kamwe hawakuwahi... walikuwa kwenye mikutano yangu hapo kabla? Hebu tuone mikono yenu. Mtu yeyote? Vema, jamani, kuna kundi lao. Hujawahi kuona mmoja wa mikutano hiyo? Vema. Wote walio humu jengoni wanaojua wakati nilipoanza kutoka kwa mara ya kwanza kwamba mtu aliweka mikono yao juu yangu, ilikuwa ni kitu kama upambanuzi, mkononi mwangu, mkono wangu ungevimba, na vitu vidogo vyeupe vikipitia juu yake, ningeweza kuwaambia shida yao, inua mkono wako. Vema.

²⁴⁶ Ndipo nikawaambia ya kwamba yule Malaika aliyenena nami alisema itakuwa kwamba, kama nikiwa mwaminifu, nitajua siri yenyewe ya moyo wao, kama vile Musa alivyopewa karama mbili kuthibitisha huduma yake ya kuwatoa wana wa Israeli kutoka utumwani, kwamba hizi zingekuwa ni ishara mbili nilizopewa. Wakati huo nisingeweza kusema, sikujua. Halafu, baadaye, nini kilitukia? Sasa, ni wangapi waliopata kuona jambo hilo likitimia wakati huo, kwamba Yeye alijua siri yenyewe ya moyo wao? Vema, haya basi. Hizo—hizo huduma zingali zinaishi leo. Naam.

²⁴⁷ Lakini sasa, inayofuata, “Nena na itakuwa hivyo.” Lakini siwezi kunena mpaka upako uniguse, wala huo upako hauwezi kunigusa mpaka watu waamini jambo hilo. Mnaona? Hiyo imerudishwa tu mikononi mwa watu tena.

²⁴⁸ Hapa, mama huyu hapa, huyu ndiye, huyu ndiye mgonjwa? Mama, mimi sikujui. Hatufahamiani. Hiyo ni kweli?

²⁴⁹ Sasa iweni na kicho kwa dakika chache tu, iweni na kicho. Sasa, huyu hapa mwanamke ambaye hatujawahi kukutana naye maishani, nami simjui, wala yeye hanijui. Mungu anajua, nijuavyo mimi, sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Labda ameniona kutoka kwenye kusanyiko, lakini si—sijui.

²⁵⁰ Sasa, hebu tuone kama ile huduma ya kwanza . . . Sasa, kama ana aina yoyote ya mateso bila viini . . . Sasa mnaona, kama ni ugonjwa wa viini, huyo ni pe—pepo wa mauti. Ni wangapi wanaojua hilo? Kansa ni nini? *Kansa* inatokana na neno la Kiyunani *kaa*, linalomaanisha, “miguu mingi.” Na ni seli ndogo inayoingia ndani yako, nayo inaanza kuzidisha seli, na kujenga kitu kikubwa mno mle ndani, inainyonya damu yako, inakuua, unajua hilo, inakutia sumu.

²⁵¹ Sasa, wewe ni seli ndogo tu, pia, ulianza, ulitoka kwa baba yako, naye mama akatoa yai, ndipo ile seli ndogo ya damu ikatambaa mle ndani, ikaanza kukua, nayo ikakufanya jinsi ulivyo; mbwa, ndege, kila kitu kwa jinsi yake. Lakini hii haina umbo, ni ibilisi. Yesu aliiita . . . “Wakati pepo bubu na kiziwi alipomtoka mtu huyo, aliweza kunena na kusikia.” “Kwa Jina Langu watatoa pepo.”

²⁵² Sasa, kama huyu mwanamke ni kiwete, ama *chochote kile* kama kisukari, hicho ni kitu cha kemikali . . . Lakini kama ni—kama ni ugonjwa wa viini, nitaninii . . . itaonyesha mkononi mwangu.

²⁵³ Sasa, njoo hapa, mama. Sasa, unajua . . . unajua shida yako? Usiniambie, lakini unajua? Hujui kuna shida gani. Vema. Sasa, weka mkono wako juu ya wangu hapa, vuka upande *huu*, dada. Hiyo ni kweli. Naam, bwana, ana ugonjwa wa viini. Waweza kusogea *huku* ili niweze kuona? Naam, bwana.

²⁵⁴ Sasa, nataka wasikilizaji waone jambo hili. Nataka uangalie mkono wangu, unaonekana tu kama mkono wa mtu wa kawaida, sivyo? Sasa, mwangalie mwanamke huyu wakati anapoweka mkono wake wa kushoto, ama, mkono wake wa kulia, juu ya mkono wangu wa kushoto. Geuka *hivi*, dada, ili uulingame tu mkono wangu. Sasa, uangalie. Unaona ukifura huko juu? Unaona vitu hivyo vidogo vyeupe vikikimbia juu yake? Hivyo vinaenda hivi, “*Whirrr, whirrr, whirrr, whirrr!*”

²⁵⁵ Sasa angalia hapa. Mwangalie akiushika mkono *huu*. Weka mkono *huu* juu yake. Haiubadilishi hata kidogo, unabaki tu vile vile. Sasa ondoa mkono *huu*. Sasa wekelea mkono *huu*. Huo hapo, unaanza kufura tena. Hiyo ni kweli? Unauangalia moja kwa moja. Je, umewahi kuona jambo hilo hapo kabla? La, kamwe hujaliona.

²⁵⁶ Sasa, sasa hivi ndivyo ninavyojua shida ni nini. Sasa, weka tu mkono wako hapa, kwa dakika moja tu. Ni shida ya kike, shida ya wanawake. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ni maambukizi katika tezi ya kike. Ana jipu kwenye ovari. Hiyo ni kweli. Una maumivu, makali. Sasa, yeye pia ana tatizo la mtiririsho. Sasa, hiyo. . . Sasa, mama, sasa, siwezi kuuondoa. Unaona? Lakini kwa Roho wa Mungu, ninaweza kufanya hiyo roho iondoke humo, nawe unaweza kuiangalia. Sasa, ninawatakeni. . .

²⁵⁷ Umesikia, umehudhuria mikutano mara kadhaa na kunisikia nikihubiri? Je, unaamini kwa uchaji ya kwamba yale ninayosema kuhusu hilo ni kweli? Unaamini ile Nguzo ya Moto waliyo na picha yake, unaamini huyo ni Malaika wa Bwana kwa moyo wako wote?

Vema, sasa, uwe na kicho kabisa, sasa angalia.

²⁵⁸ Ninawatakeni ninyi. . . Nitaweka mkono wangu hapa ukitaka, mnaona, si jinsi ninavyoshikilia mkono wangu, mnaona. Njia yoyote ile, ni vile vile, sivyo? Naam, huyu mama anaangalia moja kwa moja. . . Je, mnaweza kuliona kutoka kwa wasikilizaji? Mnaona?

²⁵⁹ Sasa angalieni, ondoa tu mkono wako, angalia. Unaona, hapo unarudi kawaida. Sasa chukua mkono *huu* uuweke hapa. Wewe ni mwanadamu tu katika mkono mmoja kama ulivyo katika huo mwingine. Sasa ninawekea mkono wangu, haubadiliki hata kidogo. Sasa weka mkono wako *hapo* juu ya huo. Hilo hapo tena. Unaona? Unaona?

²⁶⁰ Sasa, hiyo inaonyesha dhahiri ya kwamba kuna kitu fulani ndani ya mwanamke huyo ambacho si sahihi. Sasa, upako wa Roho Mtakatifu uko juu yangu, ambao ni uhai. Yeye ni Mkristo, maana roho yake inajisikia kukaribishwa, mnaona, ninajua yeye ni Mkristo. Lakini kuna kitu mle ndani kinachojaribu kumtoa uhai, huyo ni ibilisi. Sasa, hilo si ni zuri sana? Halafu basi, pasipo mimi kufanya chochote, ninaliacha tu litendeke. Anarudi. . .

²⁶¹ Sasa angalieni hapa sasa, ili kwamba upate mtazamo mzuri. Sasa, ninakutaka, wewe mwenyewe, uangalie huo mkono. Sasa, kama ikitoka, sawa. Isipotoka, bila shaka si—siwezi. . . Sasa, kama utaamini sasa, unaona, hilo ndilo ninalokuuliza, utaamini kama akiondoka, kwamba hatarudi. Uta—utadumisha imani huko juu, na kuendelea. . . “Pepo mchafu akimtoka mtu, hutembea mahali pasipo na maji.” Hiyo ni kweli? “Anarudi tena. . .”

²⁶² Tuseme jambo fulani limetukia. Billy, ndiyo kwanza nione ni nini. . . Leo, ndio kwanza nione kwenye saa yangu. Mimi. . . Hii ni saa ya mkononi ya dola mia tatu waliyonipa huko Uswisi. Nayo, Loyce, mwajua, na Becky, mwajua, haijaonyesha saa vizuri kwa siku nne ama tano zilizopita, imekuwa ikienda mrama. Ndiyo kwanza niisikie ikisimama papo hapo tena. Mtetemo wa kitu hicho. . . Ni wangapi wanaokumbuka hapo mwanzo jinsi ingesimama? Ni wangapi wanaokumbuka ingeisimamisha saa yangu? Hiyo hapo sasa hivi, imesimama tena. Hilo ndilo linalolisababisha. Mnaona, ule mkono wa sekunde umekufa kabisa. Ilitokea tu niliwazia, hilo ndilo lililosababisha jambo hilo. Hilo hapo tena.

²⁶³ Sasa, weka mkono wako *hapa*. Na ati mtu asingeamini katika utakatifu. Vipi kuhusu hereni zote, na kadhalika, basi? Vitu visivyo vya lazima. Lakini Roho Mtakatifu anaikomesha hiyo. Kama hiyo ni ya sehemu hiyo ama sivyo, sijui. Lakini hiyo saa haitasogea, hata haitafanya kazi mradi tu. . . Na hiyo ni Kriketi ya—ya Vulcain, iliyo bora kuliko zote zinazotengenezwa na Uswisi. Walinipa hiyo ikiwa na jina langu ndani yake.

²⁶⁴ Sasa, dada. . . Sasa, ni wangapi mle ndani, katika kusanyiko hili, wanaoamini kwa uchaji na wanajua ya kwamba jambo fulani linatukia hapa? Kama ungeweza kuliona. . . Laiti ningalikuwa na wakati kwa ajili ya kila mmoja wenu anayepitia hapa. Kuna mtu yeyote humu jukwaani hajawahi kuiona? Nyote mmeiona, nadhani. Umeiona, wewe, wewe. Umeiona, Roy? Njoo hapa.

²⁶⁵ Roy ni mmoja wa washirika wetu wapya. Sasa, Ndugu Roy, angalia mkono wangu. Unaonekana tu wa kawaida, nikiweka mkono wangu juu yake, unaonekana wa kawaida. Unaona? Nikiweka mkono wake, mkono *huu*, unaonekana wa kawaida. Sasa, weka mkono *huu* hapa uone kitakachotukia. Huo hapo. Unaona ninalomaanisha? Unaona jinsi unavyofura, na vitu hivyo vidogo vinanivamia?

²⁶⁶ Sasa, hayo ni mauti yaliyo ndani yake, yakiutetemesha uhai, nao uhai ukiyazuia. Sasa, ni kipi kilicho na nguvu zaidi, uzima au mauti? Uzima. Ni kipi kilicho na nguvu zaidi, nuru au giza? Haidhuru nuru ni ndogo jinsi gani, itaangaza gizani. Kwa hiyo basi, nguvu za Mungu zina nguvu zaidi kuliko nguvu za mauti, kwa sababu Yeye ni uzima. Ni kipi kilichotangulia, uzima au

mauti? Uzima. Mauti ni nini? Uzima uliopotoshwa. Udhalimu ni—ni nini? Dhambi ni nini? Haki iliyopotoshwa.

²⁶⁷ Hapa, huenda ukajua jambo hili, unaishi na mke wako kama mke. Hilo ni halali, hilo ni zuri, hilo ni sawa, takatifu, kitanda ni safi; tendo lile lile na mwanamke mwingine, unaelekea jehanamu. Ni kitu gani? Haki iliyopotoshwa. Unaona?

²⁶⁸ Sasa, sawa na hili. Sasa, mwanamke huyu hapa ana roho ya Uzima ndani yake kama Mkristo, ana roho ya mauti ndani yake kama kiini. Hiyo hatimaye ingesababisha kansa, angekufa, iyachukue maisha yake, impeleke kwenye kaburi la mapema. Sasa, kama utaamini kwa moyo wote... Njoo hapa, Roy. Hata hivyo... Kama utaamini kwa moyo wako wote... Anasema ataamini. Itamsaidia. Wewe—wewe angalia mkono wangu, Roy. Wewe angalia mkono wangu.

²⁶⁹ Na laiti ninyi, hasa ninyi wanawake, mngeinamisha vichwa vyenu, maana kitu hiki, kitakapotoka, kitaenda mahali pengine. Ni wangapi wanaojua hilo? Biblia ilisema hivyo. Kitaenda mahali pengine kama kinaweza kuingia mahali pengine. Sasa, nitaushika mkono wangu namna *hiiyo* tu, Roy, kamwe usiusogeze. Sasa, angalieni kama itatoka. Kila mtu awe na kicho sasa, iweni katika maombi.

²⁷⁰ Baba wa Mbinguni, sijui ni lini ningeweza kurudi kwenye Maporomoko, Maporomoko ya Klamath tena. Natumaini mara moja, Bwana. Lakini kama ningerudi katika mwaka mmoja, kuna wengi hapa, kama nikiishi, hawatakuwa hapa, wataondoka. Nami nataka hii iwe ishara ya hakika, ya kwamba kila kitu ninachoweza kufanya, wapate kujua ya kwamba Mungu ni Mungu. Nami ninamwomba mwanamke huyu, na kuomba ya kwamba kitu hiki kiovu ambacho kiko karibu kuyachukua maisha yake kitatoka na kumwacha. Tujalie, Baba, katika Jina la Yesu, Mwanao.

²⁷¹ Sasa, hakijamwacha, maana kingali kinagongagonga mkono wangu; sijafungua macho yangu, Mungu anajua. Lakini, Ndugu Roy, ungali unavimba na kukimbia kama—kama ilivyofanya. Dada, kabla sijafungua macho yangu, ungali unavimba, sivyo? Ungali tu kama ulivyokuwa. Hakikutoka.

²⁷² Sasa, ili mpate kujua ya kwamba Neno la Mungu ni kweli, sasa, kama mwanamke huyu... Sijaingia katika upambanuzi pamoja naye. Lakini nikiamini kwamba yeye ni Mkristo na ameomba kabisa... Sasa—sasa, Mungu hutupa nguvu si kuponya, bali kutoa roho. Sasa, weka jicho lako hapo uone kama kitaondoka. Sasa, Roy, wewe angalia uone, ama yeyote wenu, anayetaka kuangalia, angalieni kama mkono wangu utasogea, ama chochote kile.

²⁷³ Baba wa Mbinguni, ili ulimwengu upate kujua, hatuombi miujiza, kizazi dhaifu na cha zinaa kinafanya hivyo, bali

kwamba ulimwengu upate kujua ya kwamba Wewe ungali unalitimiza Neno Lako:

²⁷⁴ Ninamwamuru ibilisi huyu anayemsumbua dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, atoke ndani yake!

²⁷⁵ Sasa, huyo hapo ametoka. Sasa, kabla sijafumbua macho yangu, mkono wangu umegeuka kuwa mweupe kutoka kwenye mwekundu-samawati, yale madoa madogo meupe yamekoma. Hiyo ni kweli? Fungueni macho yenu, kila mtu. Sasa, nitajiangalia mwenyewe. Haya basi. Sasa, nyote mnetafuta jambo hilo, ndugu? Jambo fulani lilitukia, sivyo?

²⁷⁶ Sasa angalieni hapa, nitauchukua mkono *huu* na kuuweka *hapa*. Mnaona jinsi unavyoonekana? Ninachukua mkono *huu* na kuuweka *hapa*. Angalia hapa, dada, sawa tu na huo mwingine. Mnaweza kuuona kutoka hapo?

²⁷⁷ Sasa, ni jambo gani lililotukia? Ibilisi alitolewa, huyo mwanamke yuko huru, anaweza kwenda zake akishangilia. Hiyo ni kweli. Sasa, ameliona, wahudumu hawa wameliona, nanyi kutoka hapo mliona jambo hilo, mliamini neno letu kwamba ni kweli. “Kama tu utaamini!”

²⁷⁸ Njoo, mama. Sasa kila mtu awe na kicho. Hebu tumwone mwanamke huyu hapa. Hebu tuone tu mkono wako kwa dakika moja, kabla hatujaanzisha mstari wa maombi, hebu tuone mkono wako. Geuza mkono wako namna *hii*. Sasa, sikujui, kwanza. Hivi hatufahamiani? Tumezaliwa umbali wa maili kadhaa, tukaachana kwa miaka kadhaa, wewe ni mdogo sana wa umri kwangu, lakini hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana. Naam, bwana, ana u—ugonjwa wa viini. Naam, bwana. Ugonjwa wa tumbo. Unaamini kwa moyo wako wote kwamba Bwana Yesu anaweza kukuponya na kukupa afya? Unaamini.

²⁷⁹ Sasa nataka uangalie. Sasa ondoa mkono wako kutoka kwa wangu. Sasa angalia jinsi mkono wangu unavyogeuka. Sasa hebu nichukue lesu uliyotaka mtu fulani. . . Sasa ngoja, upindue *huu*. Sasa angalia hapo. Ni wa kawaida tu, sivyo? Sasa rudisha lesu yako hapa. Sasa chukua mkono *huu* na uugeuze moja kwa moja *hapa* ndani. Sasa uangalieni ukivimba. Mnaona? Mnaona vitu hivyo vidogo vyeupe vikipita juu yake? Sasa, hiyo ni kutokana na mtetemo, ambapo ugonjwa wa vidonda ungemfanya ku—kuvuja damu, ama chochote kile, Mnaona.

²⁸⁰ Sasa, sasa, siwezi kumponya huyu mwanamke, bali kwa karama ya Mungu ninaweza kumfanya yule mwovu kumwacha. Wewe ni Mkristo? Umeomba kabisa? Utampa Mungu sifa? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini hili kuwa ni kweli? Vema. Sasa angalia mkono wangu. Mtu yeyote anayetaka, kama unataka kuutazama, unakaribishwa hata na zaidi.

²⁸¹ Ninawatakeni mwone, si hali ya mkono, ama chochote kile, ni kama tu ulivyokuwa.

282 Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu. Sasa, kama una mzio kidogo wa ugonjwa wa tumbo, huu unasababishwa na hali ya wasiwasi. Sasa—sasa, kama mtaviinamisha tu vichwa vyenu kwa dakika moja tu.

283 Baba yetu wa Mbinguni, si kwamba ingekuwa ni maonyesho ya hadharani, bali kwamba watu hawa wanaosimama kwenye mstari huu wa maombi wapate kuwa na imani ya kuombewa na kuponywa, na ijulikane, Bwana, ya kwamba Wewe ni Mungu nami ni mtumishi Wako. Ninaomba ya kwamba utalithibitisha Neno Lako leo kwa kuwatoa pepo wachafu.

284 Bwana, mwisho umekaribia, wakati unakuja, na watu hawana budi kujua yakini ya kwamba sisi, Wakristo, tunajua ya kwamba tumaini letu halijajengwa juu ya kitu fulani cha kisiri, bali kabisa, juu ya Neno la Mungu na Mungu ambaye anaweza kufanya mambo yote yatende kazi pamoja kwa ajili yetu. Sasa, Baba, nimekuomba Wewe uwe pamoja nami na kunisaidia, ninapoenda, kwa imani, kumpa changamoto ibilisi huyu ambaye amemdhuru dada yangu.

285 Shetani, ninakuamuru kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kwa kufufuka Kwake na ushindi juu yako, alikunyang'anya mamlaka yote ya kisheria, wewe si kitu ila mdanganyifu, tunakupa changamoto, kwa karama ya Mungu niliyopewa, iliyohudumiwa na Malaika, ninakuamuru, katika Jina la Yesu, toka ndani ya mwanamke huyu, mwache, na umwachilie!

286 Sasa, aliondoka. Kama akiondoka, mkono wangu umeacha, sijawahi kuuangalia, lakini umeacha kutetemeka. Hiyo ni kweli? Huo hapo. Huo hapo, mnaona? Uligeuka kawaida. Sasa amekuacha. Nenda zako ukashangilie, na kusema, “Asante, Bwana,” na upate afya.

287 “Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana kwao ambao. . .” Unaliamini? Sasa, mwaminini Mungu. Ni wangapi huko nje. . .? Sasa, hiyo ni karama moja inayofanya kazi kwa hiyo. Sasa kwenye karama nyingine. Unaamini kwa moyo wako wote? Ni wangapi huko nje walio wagonjwa, ama una shida fulani? Inua mkono wako, ili kwamba tu mpate kujua kabla hatujawaombea wagonjwa. Mungu anisaidie.

288 Sasa, iweni na kicho, kaeni kimya. Haidhuru uko wapi, roshani, juu na chini kwenye safu, haidhuru, haijalishi hata kidogo, wewe endelea tu kuamini. Iweni tu na kicho.

289 Sasa, usi—usijifanye. . . Unashikwa na wasiwasi, jitulize tu, useme, “Bwana, naamini.” Useme, “Sifahamiani na huyu mtu, hebu aniambie, nami nitaamini kwa moyo wangu wote kama angeniruhusu tu niseme, ama, aniambie.”

290 Iweni na kicho kabisa, kila mtu. Unaona, kila wakati unaposogea, roho yako, unaona, nina mahali pako, mahali ulipo, nikihisi mtetemo wako, ndipo unapo—unaposogea, basi inamkatiza Roho, unaona, nami silipati.

²⁹¹ Hapa, huyu hapa mtu ameketi pembeni, papa hapa. Inaonekana kana kwamba ninaujua uso wake, sikumbuki yeye ni nani. Je, uliinua mkono wako dakika chache tu zilizopita? Uliinua. Vema, unajua sijui una shida gani. Sina njia ya kujua, lakini unaamini ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, anaweza kunifunulia shida yako, bwana? Unaonekana kuwa... Una kivimbe. Hiyo ni kweli. Hicho kivimbe kiko kwenye sikio. Unaamini kwa moyo wako wote sasa, ya kwamba atakuponya? Vema. Amini.

²⁹² Hilo kidogo lilikutikisa, mama? Vipi kuhusu hiyo mishipa iliyovimba? Unafikiri ya kwamba Mungu angeponya mishipa hiyo? Huh? Unafikiri? Uko tayari kufanyiwa upasuaji wake juma hili. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama. Vema. Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani, mara tu nilipozungumza na mtu huyo, Kitu fulani kilikugusa. Hiyo ilikuwa ni kweli? Kama ndivyo, pungu mkono wako.

²⁹³ Ni kwa sababu Nuru hiyo ilitoka papo hapo juu ya huyo mwanamume, moja kwa moja mpaka kwa huyo mwanamke. Sijui hata mmoja wao, ila ni—nilimwona mtu huyu mahali fulani, siwezi kujua yeye ni nani, bali nimeuona uso wake, bali sijui yeye ni nani, lakini Yesu Kristo anamjua, Anajua yote kumhusu. Yeye ni Bwana Yesu yeye yule, yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaamini kwa moyo wako wote?

²⁹⁴ Huyu hapa mama ameketi hapa ameinamisha kichwa chake, sijawahi kumwona maishani mwangu. Lakini yeye anaomba, “Bwana, acha iwe ni mimi.” Huyu mwanamke, ana shida miguuni, pia ana ugonjwa wa moyo. Pia anajiomba mwenyewe. Asipoikosa! Mama huyo, loo, jamani, mama huyo hatoki hapa, anatoka California, jina lake ni Bi. Goodwin. Unaamini sasa? Simama kwa miguu yako kama hiyo ni kweli, kama kila sehemu yake ni kweli, nawe ulikuwa umeketi ukiomba hilo, inua mkono wako. Hivi hatufahamiani, sisi kwa sisi? Punga mkono wako namna *hii*. Vema, rudi nyumbani kwako, Yesu Kristo anakuponya.

²⁹⁵ Kama hawataamini *hii*, wataamini *ile*; hawana budi kuamini *ile*. Loo, laiti mngaliweza tu kuamini! Kama unaninii...

²⁹⁶ Kuna mama aliyeketi papo hapo nyuma akiniangalia, naye ana—ana uvimbe kwenye titi lake la kushoto. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, mama, na kukupa afya? Kama unaamini kwa moyo wako wote! Vema.

²⁹⁷ Huyu hapa mama mwingine aliyeketi papa hapa nyuma, la, anamwomba mwanamume. Ni shemeji yake, ana kansa ya koo. Unaamini ya kwamba Mungu atampa afya? Liitikie upesi, kama huninii... Vema.

298 Nilimwona mtu huyo akitoweka, mnaona. Inakubidi, unapoitwa, kujibu upesi. Usiwe na shaka, amini kwa moyo wako wote.

299 Mwanaume uliyeketi huko nyuma ukiwa na ugonjwa wa pumu, kukohoa. Unaamini Mungu atakuponya? Unaamini kwa moyo wako wote? Kama unaweza kuliadini, vema. Bw. Lowe, basi Mungu atakuponya kama utaadini.

300 Kwa nini inanibidi kuliita jina lako? Unaamini hilo? Kila mtu, kuwa na imani. Mwamini tu Mungu.

301 Unataka kuondoa ugonjwa huo wa tumbo, bwana, huko nyuma unayeumwa na tumbo lako? Iwapo unataka, acha kuvuta sigara hizo, naye Mungu ataponya tumbo lako. Amina.

302 Unaamini kwa moyo wako wote? Ni wangapi wanaoamini sasa kwa moyo wako wote, useme, “Ninaamini ya kwamba Bwana Yesu Kristo atawaponya wagonjwa.”

303 Unaonaje? Unaamini ugonjwa wa mgongo utakuacha, na Mungu akupe afya, utaenda nyumbani, uwe mzima? Vema, nenda zako na uamini kwa moyo wako wote. Vema.

304 Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini ugonjwa huo wa moyo utapona? Unaamini utakuwa sawa? Mhubiri mwanamke anapaswa, kwa vyovyote vile, kama unaamini kwa moyo wako wote, nenda zako.

305 Sasa angalia, ninaanza kujisikia dhaifu sasa hivi. Nina wengi kupita kiasi mstarini. Ni wangapi wanaoamini? Kama karama ya kwanza inafanya kazi, karama ya pili inafanya kazi, ya tatu haina budi kufanya kazi, ni Mungu. Sasa, ni wangapi wenu kwenye mstari huu wa maombi huko nje tayari wameomba kabisa, na kuamini ni mapenzi ya Mungu kukuponya? Inueni mikono yenu.

306 Mama, umeomba kabisa, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Basi sina kitu cha kufanya, ila tu kumtoa ibilisi, na kumwacha aendelee na awe mzima. Tayari ameomba kabisa, sivyo? Hiyo ni kweli?

307 Sasa, ni wangapi wenu wataungana nami katika maombi, kwamba kila mmoja wa watu hawa watakapokuja kwa kuwawekea mikono, watapata afya? Mnaamini hilo? Vema, nyote piteni kwa moyo wenu wote sasa, tembeeni tu kwa uthabiti, sawa.

308 Sasa, hebu kidogo, kabla ya hapo, ninajaribu kupata huo upako...Ni vigumu sana kuliondoa mara likija kwa kusudi hilo. Ninaona mtoto akiendelea kutokea mbele zangu, hapa, inaonekana kama mpasuko ama kitu fulani kwa huyo mtoto. Ni *wewe*, unayemwombea mtoto mchanga hapo.

309 Ninakupa changamoto kumwamini Mungu. Ninawapa changamoto kumwamini Yeye. Msiogope, ni Kristo, Mwana wa Mungu. Msiogope, aminini tu, mambo yote yanawezekana.

Njoo sasa, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, ibilisi na amwache.

Njoo, ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamtoa ibilisi huyu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamtoa huyu mwovu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamtoa huyu mwovu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamwondoa huyu mwovu kutoka kwa huyu mtoto.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamtoa huyu mwovu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamtoa huyu mwovu.

³¹⁰ Mnaamini hao watu wataponywa? Hakika. Unaamini? Ninyi ambao mmepitia mstarini? Watapata afya? Mnaamini hilo? Iweni na imani sasa, Ninataka kuona kama kitu fulani kinarudisha mwangwi. Iweni katika maombi sasa, kila mtu katika maombi. Na unapopitia hapa, amini, usipofanya hivyo, haitafaa kitu. Vema.

Ninamwondoa yule mwovu kutoka kwa ndugu yangu, katika Jina la Yesu.

Njoo, dada. Amini sasa.

Ninamwondoa yule mwovu kutoka kwa dada, na kumbariki, katika Jina la Yesu.

Ninamtoa yule mwovu, na kuomba baraka za Mungu, katika Jina la Yesu.

Ninamtoa yule mwovu kwa kumwekea mikono, “Katika Jina Langu, watatoa pepo,” alisema Yesu. Amina.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamtoa yule mwovu kutoka kwa ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaondoa uovu kutoka kwa watoto na huyu mtoto mdogo.

³¹¹ Mungu ambariki. Haikukua vizuri sana, huh? Unaamini itanyoshwa? Itakua sawasawa ukipenda. Naam, naam, najua. Unaona, kama nikianza hiyo, inaendelea tu kusonga mbele, na kuendelea; ninajaribu kutumikisha huduma nyingine. Lakini sasa, sikiliza, niamini kwa moyo wako wote, watoto wako watapata afya. Unaamini hilo? Mungu amekupa ulichoomba, sasa, kwa hiyo nenda ukaamini. *Ulikuwa* na huo. Hutakuwa nao tena ikiwa tu utaamini.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamtoa yule mwovu.

³¹² Sasa, jambo ni kwamba, maskini mama huyo kidogo alikuwa dhaifu katika imani, Ilinibidi tu kumwambia kuhusu watoto, kusudi impe imani, hivyo tu. Mnaona? Vema.

Bwana, katika Jina la Yesu, ninamwombea dada yangu na kumtoa yule mwovu, katika Jina la Yesu.

Ninamtoa yule mwovu kutoka kwa dada huyu, katika Jina la Yesu.

Ninamtoa yule mwovu kutoka kwa dada yangu, katika Jina la Yesu.

Ninamtoa yule mwovu kutoka kwa dada yangu, katika Jina la Yesu.

Bado unafikiri una wito? Huh? Unafikiri unataka kuihubiri Injili?

Bwana, msaidie huyu mtoto, naomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki.

Ubariki maskini moyo wake. Aliomba dua kwa ajili ya baba yake. Ubariki maskini moyo wake. Mungu akubariki, kipenzi. Mungu amshughulikie baba, amrudishe.

Mungu, katika Jina la Yesu, mponye dada yangu.

Mponye ndugu yangu, Mungu, katika Jina la Yesu.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yangu.

Ee, Mungu, mponye dada yangu, katika Jina la Yesu.

Mponye ndugu yangu katika Jina la Yesu.

Mponye dada yangu, katika Jina la Yesu.

Mponye ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo.

Mponye dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo.

Mponye maskini ndugu yangu hapa (Unafikiri itakuacha?), katika Jina la Yesu.

Mponye dada yangu, Mungu, katika Jina la Yesu.

Mponye huyu, dada yangu, katika Jina la Yesu.

Mponye huyu, dada yangu, Baba, katika Jina la Yesu.

Mponye huyu, dada yangu, ninamtoa yule mwovu kutoka kwake, katika Jina la Yesu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamtoa yule mwovu.

Katika Jina la Yesu Kristo, minamtoa yule mwovu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamtoa yule mwovu kutoka kwa ndugu yangu.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninamtoa yule mwovu kutoka kwa ndugu yangu. Amina.

³¹³ Mnaamini waliponywa? Je, Biblia inasema hivi? Sasa, hebu tuchukue tu jambo hili kwa muda kidogo tu. Je, Mungu anaweza kukosea? Mungu anaweza kusema uongo? Mbona, haiwezekani, sivyo, marafiki? Haiwezekani kabisa kwa Mungu kusema uongo.

314 Sasa, yule mama aliye na yule mtoto mchanga yuko? Sasa, kwenu ninyi ambao ndio kwanza mpitie kwenye mstari huu wa maombi, hivyo ndivyo mtoto huyo mchanga alivyopitia kwenye mstari wa maombi, juma moja lililopita, leo. Hiyo ni kweli, dada? Vema. Mlisikia mahubiri yangu, jinsi nilivyotaja jambo kama hilo? Sasa, huyo hapo maskini mtoto mchanga akienda zake akiwa mzima, akipona kabisa. Sasa, angalieni tu, kama jambo lilo hilo halitukii kwenu.

315 Sasa, mnaona, marafiki, Mungu anaweza kwenda kiasi fulani, umbali fulani, bali huna budi kukutana Naye kwenye maeneo hayo huko. Unaamini?

316 Unafikiria nini juu yake? Wewe. Unafikiri tumbo litapata afya, litapona? Huyo ni mke wako aliyeketi hapo, kidogo amelala, kitu kama ugonjwa, ama kitu fulani. Hiyo ni kweli. Una ugonjwa wa tumbo, na wewe ni mhubiri. Unaamini Injili. Hiyo ni kweli? Sijawahi kukuona maishani mwangu, hatufahamiani kabisa. Je, hiyo ni kweli? Kuna Nuru moja kwa moja juu yako, ninaiangalia. Sasa, inua mkono wako kama hiyo ni kweli, nyote wawili. Weka mkono wako juu ya mkeo; mke, weka mkono wako juu yake.

317 Shetani, umefichuliwa. Toka kwa hao watumishi wa Mungu, Ninakuamuru, katika Jina la Yesu Kristo, uwaondokee!

318 Haya basi. Sasa, pumzika kwa amani.

319 Unaona hapo? Mtu huyo aliyeketi hapo, sijawahi kumwona maishani mwangu, na hapo Roho alimshika, moja kwa moja namna hiyo. Nami nikaona Nuru hiyo ikimulika kote jengoni, nikaiangalia, nikawazia, “Hiyo ilikuwa ni nini? Uakisi fulani huko nje?” Nami nikaangalia, hii hapa Nuru ile inakuja ikitua moja kwa moja juu yao, ndipo ono likatokea juu yao. Sijawahi kuwaona maishani mwangu. Hawakuwa kwenye mstari wa maombi.

320 Hu—hukuwa katika mstari wa maombi, sivyo, bwana? Hukuwa na kadi ya maombi wala chochote kile. La, maana hakuna kadi za maombi zilizotolewa. Kwa hiyo basi, kadi zote za maombi zimekwisha. Mnaona? Kwa hiyo, haya basi.

321 Mnaona? Ni imani yako tu katika Mungu. Kristo angeweza kufanya nini cha zaidi? Anaweza kuja hapa na kunyosha mikono Yake, na kusema, “Mimi Ndiye. Msiogope, Mimi Ndiye, niaminini Mimi mpate kuponywa.” Je, hiyo ni kweli?

Loo, hivi hamupendi? Yeye si ni wa ajabu?

Yeye si ni wa ajabu, wa ajabu, wa ajabu?

Je, Yesu Bwana wangu si ni wa ajabu?

Macho yameona, masikio yamesikia, yale yaliyoandikwa katika Neno la Mungu;

Je, Yesu Bwana wetu si ni wa ajabu?

Hebu sote tuuimbe pamoja.

Yeye si ni wa ajabu, wa ajabu, wa ajabu?
 Je, Yesu Bwana wangu si ni wa ajabu?
 (Sikilizeni sasa, yale Yeye aliyosema.)
 Macho yameona, masikio yamesikia, yale
 yaliyoandikwa katika Neno la Mungu;
 Je, Yesu Bwana wangu si ni wa ajabu?

322 Loo, hebu na tuinue tu mikono yetu na kumsifu.

323 Ee Bwana, Ua la Uwandani, Nyinyoro ya Bondeni, Nyota ya Asubuhi, Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho, Yeye Aliyekuwako, Aliyeko, na Atakayekuja, Shina na Mzao wa Daudi, Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele, Wa Ajabu!

324 Loo, jinsi tunavyokushukuru na kukusifu Wewe, Bwana wetu, kwa wema Wako na rehema Zako kwa watoto wa wanadamu! Jinsi tunavyokusifu na kukutukuza, Wewe mwenye haki na, kweli, Mwana wa Mungu! Tunakushukuru kwa yale macho yetu yameona, masikio yetu yamesikia.

325 Macho yetu yamemwona Roho Mtakatifu. “Jamani,” mshairi alisema, “macho yangu yameuona utukufu wa kuja kwa Bwana.” Kwa kweli, Bwana, masikio yetu yameisikia Sauti Yako ikinena, tukaiona ikitenda kazi na kufanyika kwamba pepo wanakutii. Ee Bwana, pepo wanatiishwa chini ya Jina Lako, pepo wanatiishwa chini ya nguvu Zako. Na siri za mioyo zinafunuliwa, wagonjwa wanaponywa, watu wanaoteseka wanapata afya, vipofu wanaona, viziwi wanasikia, viwete wanatembea, wafu wanafufuliwa, Kuja kwa Bwana kumekaribia. Jinsi tunavyokushukuru Wewe, Bwana!

326 Mungu bariiki Maporomoko ya Klamath, Bwana. Mimina Roho Yako juu ya hawa wahudumu na wachungaji hapa, Mungu, juu ya Kanisa Lako, juu ya miji yote jirani huku. Okoa kila nafsi inayoweza kuokolewa, Mungu. Tujalie. Ninaamuru kwamba Wewe... Tujalie.

327 Halafu, Baba, leso hizi zilizowekwa hapa, zinawakilisha wagonjwa, mtu fulani, mahali fulani, anayeteseka. Wakati leso hizi zinapokuja juu ya watu, jalia Roho Mtakatifu aje juu yao na kuyaponya magonjwa yao. Tujalie, Bwana. Tunakushukuru na kukusifu Wewe kwa yote ambayo umetenda.

328 Na kama kuna mmoja hapa, Bwana, bado, ambaye hana imani baada ya kukuona Wewe, jalia wasijisikie kwamba ni mzuka ama kuna kasoro fulani, jalia wasikie hiyo Sauti tamu ikisema, “Msiogope; Ni Mimi; iweni na moyo wa ushujaa.”

329 Nao, na hebu wakukaribishe kwenye jahazi lao dogo alasiri ya leo, wataenda nyumbani kwao wakishangilia na kumsifu Mungu, wakisema, “Tumemwona.” Kama wale waliotoka Emau baada ya kutembea na kulia mchana kutwa na usiku kucha, kujua ya kwamba ulikuwa umekufa, na kuwekwa kaburini, na kuzikwa; ndipo ukatembea pamoja nao. Na ndipo ulipowaweka

chumbani peke yao, ulifanya jambo fulani kama tu ulivyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, nao walijua ya kwamba Wewe pekee ndiwe uliyefanya hivyo, kwa hiyo wakatambua ilikuwa ni Wewe.

³³⁰ Umetufanyia jambo lile lile, leo. Baada ya miaka elfu mbili, Wewe huyu hapa leo mkutanoni ukifanya jambo lile lile ulilofanya kabla ya kusulubiwa Kwako. Hakika, Wewe hujafa, Bwana, U hai milele, umefufuka katika wafu, ukawashinda wafu. Adui Zako wote wakifanywa kitu cha kuwekea miguu Yako, Nawe unatoa nguvu Zako kwa Kanisa Lako, na kwa watu Wako. Wewe—Wewe ulipaa Juu na kuwapa wanadamu vipawa. Na sisi hapa katika wakati wa mwisho, Nuru za jioni zikiangaza. “Itakuwa Nuru,” alisema mshairi, “wakati wa jioni, njia ya Utukufuni hakika mtaipata.”

³³¹ Ee, Mungu, jalia watu wapate njia hiyo na watembe ndani yake. Tunakushukuru kwa ajili ya kila mtu ambaye ameipata, nasi tunakusifu kwa ajili yake. Mponye kila mgonjwa aliye mjini, kila mtu aliye hapa kanisani. Kama kuna mmoja hapa, kwenye roshani, popote pale aliye mgonjwa au anayeugua, hebu maombi yangu na yawafanye upatanisho, wakati upako wa Roho Mtakatifu ukiwa juu yangu.

³³² Hebu Roho wa Mungu, awezaye kuyatambua mawazo ya moyo . . . Kama Biblia ilivyosema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, hata huchoma na kugawanya mafuta ya mfupa, na ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo.”

³³³ Sasa, Neno la Mungu ni nini? “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Huyu hapa katika ufufuo leo, akiishi miongoni mwetu, Neno likihibiriwa kwa nguvu za Roho Mtakatifu na kuyatambua mawazo ya moyo. Haleluya! Jina la Bwana libarikiwe.

³³⁴ Jalia watu walione, Bwana, kabla haijachelewa sana. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

³³⁵ Mnaamini? Unaamini kwa moyo wako wote? Unaweza kulikubali? Ninakukabidhi kwa Yesu Kristo, Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu, na kwa mchungaji kama mtumishi wa Mungu. Mungu awabariki, mpaka nitakapowaona tena. 

60-0717 Msiogope
Shule Ya Sekondari Ya Juu Ya Klamath Union
Klamath Falls, Oregon Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org